# Nipashe

Jumatatu Septemba 12, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581066

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




UKURASA 11








## Wanywaji wa maziwa mikoa hii hatarini

UKURASA 15

# Bima ya Afya sasa kwa wote



• **Samia** aanika kila kitu, mkakati kuinusuru NHIF... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**ASKOFU AWAONYA WANAOSAKA MIUJIZA**

ASKOFU Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki Dar es Salaam, Thaddaeus Ruwa'ichi...

UKURASA WA 7

**MISA TANZANIA YASISITIZA UMUHIMU KUBADILI SHERIA**

TAASISI ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Jangwa la Sahara, Tawi la Tanzania...

## Mifuko plastiki yageuka kitendawili

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akiangalia bidhaa kwenye mabanda ya maonesho ya Umoja wa Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA) kutoka majimbo mbalimbali nchini, baada ya kuwasili Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana kwa ajili ya kushiriki Jubilee ya miaka 50 ya jumuiya hiyo tangu kuanzishwa kwake. **PICHA: IKULU**

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, akimkabidhi mfano wa hundi Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa (ALAT), Sima Constatine Sima, ikiwa ni udhamini wao katika mkutano mkuu wa jumuiya hiyo unaotarajiwa kuanza leo. NMB imekuwa mdhamini mkuu wa mkutano huo na imetoa jumla ya Sh. milioni 120. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**




## Serikali yatoa angalizo video, picha zenye maudhui ya ushoga, usagaji

UKURASA 3

**MICHEZO** **NABI ALIA KUPOTEZA NAFASI** UK.24

**KABWELA** UK.18

## Askofu awaonya wanaosaka miujiza

**Na Mwandishi Wetu**

ASKOFU Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki Dar es Salaam, Thaddaeus Ruwa'ichi, amewataka wanawake nchini kutokubali kuyumbishwa na makanisa ya miujiza yanayoibuka kila kukicha.

Katika misa ya kilele cha Jubilee ya Miaka 50 ya Chama cha Kitume cha Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA) mkoani Dar es Salaam jana, Askofu Ruwa'ichi alisema ndani ya kanisa hilo hawajapungukiwa kwa kuwa kuna hazina zote za utakatifu wanaouhitaji kwa ajili ya wokovu.

"Zingatieni hazina mnayoipata ndani ya kanisa lenu Katoliki maana ni hazina kubwa, itafuteni hazina hiyo na muwe wajumbe wa kuipeleka kwa wengine," alisema.

Askofu Ruwa'ichi alisema kuna tatizo kubwa linalowakabili kinamama wengi kwa sasa, sehemu kubwa wakiwa ni vijana na watoto wanaojilea wenyewe, akisisitiza kuwa 'ni hatari sana'.

"Ninaomba niwaangalishe kinamama, hiyo ni hatari na haina tofauti na yule anayelima shamba lake kisha haliangalii wala kulitunza, mwisho wa siku hutegemea kuvuna mabua, hivyo kinamama tafakarini hili la malezi," alitoa angalizo.

Kiongozi huyo wa kiroho pia alisema anamshukuru Mungu kwa anayoyatenda ndani ya kanisa hilo kupitia kuwapo wanawake Wakatoliki.

"Pia tunamshukuru Mungu kuwa na kanisa lenye uhai wa vijana wengi, ambao zaidi ya asilimia 70 ni watoto na vijana, hii ni baraka, hivyo jukumu lenu kinamama kushirikiana na waume zenu kuhakikisha mnawapatia hawa watoto na vijana malezi ya imani na yenye maadili," alisema.

Rais wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Gervas Nyaisonga, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwaamini wanawake na kuwapa nafasi za kuongoza katika kada mbalimbali, huku akiomba radhi kwa niaba ya wanawake waoshindwa kufanya vizuri kwenye nafasi mbalimbali, akiamini wataendelea kufanya vizuri katika kujenga nchi.

"Ninawashukuru na kuwapongeza WAWATA na wanawake wote Tanzania, kwamba katika miaka yote 50 wameonyesha ujasiri, ustahimilivu na umakini mkubwa kukabiliana na shida ambazo nchi imezipitia kwa miaka yote. Katika nyakati zote wameonyesha umahiri mkubwa na ujasiri, wamekuwa sababu ya furaha na matumaini kwa Watanzania wote, ndiyo maana Tanzania inaendelea kushamiri," alisema.

Askofu Nyaisonga alisema ukimwezesha mwanamke umeliwezesha taifa na wengi wanaamini kwenye karama hiyo.

# Bima ya Afya sasa kwa wote

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema mkutano wa Bunge utakaoanza kesho, pamoja na mambo mengine, utapitia na kupitisha Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote uliosubiriwa kwa muda mrefu.

Akihutubia kwenye maadhimisho ya Jubilee ya miaka 50 ya Chama cha Kitume cha Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA) jijini Dar es Salaam, Rais Samia alisema bima ya afya kwa wote itakuwa suluhisho la shida ya kupata matibabu nchini.

Alisema serikali inafahamu udhaifu uliopo kwenye mifuko ya bima ya afya na tayari imeshachukua hatua, huku akiahidi mfuko utakaosimamia bima hiyo utakuwa madhubuti, wenye sheria na kanuni mpya zitakazotoa fursa kwa watu wote kutibiwa kwa viwango mbalimbali.

"Ninataka niwape habari njema kwamba Bunge litakalokaa mwezi huu wa tisa (kesho), linakwenda kupitisha sheria ya bima ya afya kwa Watanzania wote. Niwaombe sana ndugu zangu tutakapopitisha sheria hii, Watanzania twendeni tukajiunge na mifuko ya bima.

"Ninataka niwahakikishie kwamba tunajua udhaifu uliopo kwenye mifuko yetu, tumechukua hatua. Tutakapoanza bima ya afya kwa wote, mfuko utakaosimama kusimamia bima hii utakuwa madhubuti wenye sheria na kanuni mpya ambazo zitafanya watu wote waweze kutibiwa katika viwango mbalimbali.

"Mtu apate matibabu yote anayopaswa kupata. Huu ni kama upatu ambao Watanzania wote tunakwenda kuucheza na kati yetu anayeshikwa na shida anasaidiwa na huo upatu ambao wote tumeucheza.

"Ni kupitia bima ya afya kwa wote ndipo tutaweza kutoa matibabu ya maana kwa kila Mtanzania anayeishi ndani ya nchi yetu," alisema. Akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari nchini Agosti 11, mwaka huu, Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Benard Konga, alisema magonjwa yasiyo ya kuambukiza yamekuwa mzigo mkubwa kwa mfuko huo kutokana na kutumia gharama kubwa kulipa kwa watoa huduma ya afya wanaowahudumia wateja wao. Magonjwa hayo ni sukari, figo, shinikizo la damu na saratani.

Konga alibainisha kuwa mwaka wa fedha 2021/22, mfuko huo ulitumia Sh. bilioni 99 sawa na asilimia 18 ya malipo yaliyolipwa kwa watoa huduma za afya kwa wanachama wake.

Alisema kutokana na magonjwa hayo kuwa mzigo kwa mfuko huo, aliiomba serikali kuangalia afua zingine za kitaifa za kupambana na magonjwa hayo.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, naye Septemba Mosi mwaka huu, alizungumza na vyombo vya habari huku akieleza sababu zinazochangia mfuko huo kuelemewa na kwamba miongoni mwake ni kuongezeka kwa idadi kubwa ya wananchi wenye magonjwa yasiyo ya kumbukiza ambayo gharama yake ni kubwa.

Sababu nyingine kwa mujibu wa waziri huyo ni vitendo vya udanganyifu vinavyofanywa na baadhi ya watoa huduma na wanachama wa mfuko kujipatia manufaa kinyume cha utaratibu.

Alibainisha kuwa gharama za magonjwa yasiyo ya kuambukiza zimeongezeka kutoka Sh. bilioni 35.65 mwaka wa fedha 2016/17 hadi kufikia Sh. bilioni 99.09 mwaka wa fedha 2021/22.

Agosti Mosi mwaka huu, baadhi ya wananchi katika baadhi ya mikoa walilalamika kukutana na mabadiliko kwa wategemezi wao kutakiwa kuchangia sehemu ya gharama za matibabu na kuibua mtafaruku kwa wagonjwa.



Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Zainab Chaula (wa pili kushoto), akibadilishana mkataba wa makubaliano ya ushirikiano na Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Azania, Esther Mang'enya, jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Kaimu Mkurugenzi Kitengo cha Huduma za Sheria wa wizara hiyo, Happy Msimbe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## ...Samia ataka wanawake kuchangamkia fursa kisiasa

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amekielekeza Chama cha Kitume cha Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA) kutilia mkazo mambo makuu matano ikiwamo kuchangamkia nafasi za uongozi wa kisiasa zinazojitokeza ili kutatua changamoto zinazowakabili.

Kadhalika, Rais Samia amewaondoa hofu wananchi kuwa Tanzania bado ina hali nzuri ya chakula kwa tani zisizopungua 150,000 kwa sasa zilizohifadhiwa katika ghala la akiba la chakula la serikali kwa ajili ya matumizi ya baadaye.

Alikuwa akizungumza jana katika sherehe za Jubilei ya miaka 50 ya chama hicho taifa zilizofanyika Viwanja vya Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam.

Akitaja mambo makuu hayo, la kwanza ni kuwataka wanawake kuainisha dhana halisi na ya kweli inayohusu masuala ya kisiasa na kuchagua viongozi wa kisiasa wenye sifa miongoni mwa wanawake.

"Tunajua kwamba kwenye vyombo mbalimbali vya kisiasa tumepewa nafasi maalum ya ushiriki wa wanawake, huko nako tusikuogope, twendeni kwa nguvu, tusimameni na tuhakikishe tunaowapeleka huko wanakwenda kutusemea, wanakwenda kutusaidia. Wanakwenda kusimama na masuala ya wanawake na sio ya kwao wenyewe," alisema.

Jambo la pili ni kutumia karama zao kama walezi kusimamia malezi ya watoto na vijana ili kujenga viongozi watakaoaminika na kukubalika katika jamii kuliongoza kanisa na nchi kwa ujumla.

Elimu ya uongozi kwa wanawake, alilitaja kuwa jambo la tatu ili kuwajengea ujasiri wa kujiamini na kuwa na uthubutu wa kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazowazunguka.

"Na kazi hii tumeamrishwa pia katika vitabu vyetu, ukisoma Joshua tisa inasema mwanamke ameamriwa kuwa shujaa na mjasiri, asiogope na asiwe mwenye kukata tamaa kwa sababu Mungu yupo naye," alinukuu.

Jambo la nne la tano ni wanawake kushiriki katika shughuli za kiuchumi zenye tija kwa familia na kuwa serikali ipo nyuma yao kuhakikisha hilo linafanikiwa. Kuendelea kutoa elimu kwa vijana matumizi sahihi ya teknolojia ya mawasiliano.

Akizungumzia hali ya chakula, Rais Samia alisema pamoja na mavuno hafifu msimu uliopita, Tanzania haipo katika nchi zenye hatari ya kupata baa la njaa kwa kuwa serikali ina imani chakula kilichoko kinaweza kulisaidia taifa kutoingia kwenye njaa.

"Mwaka 2019 na 2020 ghala letu lilikuwa na tani karibu 50,000 ambazo tulipoingia kwenye wakati mgumu zilisaidia Watanzania, lakini tulipata zile za kuwasaidia nchi jirani. Sasa hivi tumeongeza uwezo wa ghala letu mara tatu zaidi ya ilivyokuwa miaka miwili nyuma," alifafanua Rais.

Alisema serikali inafanya kila linalowezekana kuhakikisha kuna upatikanaji wa chakula nchini ikiwamo kutoa ruzuku kwa wakulima wahimili bei za pembejeo ili iwarahisishie katika shughuli zao.

Naye Mwenyekiti wa WAWATA Taifa, Evelyn Mtenga, alisema chama hicho kinashirikiana na serikali katika kutekeleza vipaumbele vya maendeleo ili kuifikia Tanzania wanayoitaka ikiwamo kusaidia wanawake kupambana na changamoto zinazowakabili.

Alisema pia walitoa elimu ya utunzaji wa mazingira na kupanda miti 503,416 mpaka kufikia Juni, mwaka huu ikiwa imevuka lengo la kupanda miti 34,000 ndani ya mwaka mmoja ili kuweka mazingira yenye afya kwa jamii.

Mwenyekiti huyo pia aliiomba serikali kuwasaidia watu kutoka makundi maalum kupata bima ya afya iliyo nafuu ili kuwa na uhakika wa kupata huduma na afya kwa kuwa kundi hilo bado linashindwa kumudu gharama za bima hizo.

# Serikali yatoa angalizo maudhui ushoga, usagaji

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, ametoa tahadhari kwa watumiaji wa simu janja wanaotuma na kusambaza video au picha zinazohamasisha vitendo vya ushoga na usagaji mitandaoni, kuwa hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Angalizo hilo pia linawagusa wamiliki wa mitandao ya kijamii, vituo vyenye leseni na viongozi wa makundi ya mtandao wa kijamii wa WhatsApp wasiofuta video zenye maudhui ya mapenzi ya jinsia moja.

Nape alitangaza hadhari hiyo ya serikali jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu kukithiri kwa vitendo hivyo vinavyochochewa na kukua kwa teknolojia ya mawasiliano na watu wengi kumiliki simu janja.

Alisema hatua watakazowachukulia watu wataobainika kufanya makosa hayo ni pamoja na kukamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya dola, ikiwamo mahakamani.

"Ninatoa onyo kali kwa wanaosambaza maudhui ya aina hii kwenye mitandao ya kijamii hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao kuanzia sasa. Video hizi fupi huleta taharuki kwa wananchi hasa kwa wale wapendao kudumisha utamaduni na maadili ya Kitanzania," alisema.

Nape alisema kazi ya kuwapata wanaosambaza maudhui hayo ni ya Mamalaka ya Mawasiliano (TCRA) ambayo inashirikiana na vyombo vya dola kuwachukulia hatua na kwamba zipo adhabu mbalimbali kwa mujibu wa sheria.

Alisema watumiaji wa simu wakitumiwa video hizo zisizo na maadili, wanatakiwa kufuta badala ya kusambaza kwa watu wengine kwa lengo la kuelimisha, kinyume chake inakuwa ni kuendelea kuchochea.

"Ukipata video ya namna hii kwenye simu yako, unapaswa kufuta kabisa. Usisambaze kwa sababu TCRA ina uwezo wa kukuona na kukupata wewe unayesambaza. Njia salama ni kufuta na kama una lengo la kuelimisha, andika ujumbe wa kuonya uutume na siyo utume video hiyo," alisema Nape.

Akizungumzia kukidhiri kwa matukio hayo nchini, waziri huyo alisema awali walipata malalamiko kutoka kwa wananchi kuwa vituo vilivyopewa leseni za kurusha matangazo ndivyo vinarusha maudhui hayo yasiyo na maadili kupitia chaneli mbalimbali lakini baada ya kufanya uchunguzi, walibaini wahusika ni watumiaji wa simu janja.

Alisema watumiaji wa simu hulipia maudhui hayo yanayouzwa na mitandao mbalimbali ya ndani na nje ya nchi na wakishatazama, wanazichukua video au picha husika na kusambaza kwenye makundi ya mitandao mingine ya kijamii.

"Kuwapo kwa huduma hizo za kulipia huruhusu watumiaji wa simu janja kuzipokea taarifa nyingi zinazohusu katuni za watoto na zipo zenye viashiria vya kushabikia ushoga na usagaji.

"Tukiendelea kuruhusu matumizi haya ya maudhui yasiyo na maadili, tutaendelea kuzalisha taifa la watu wasio na maadili," alisisitiza Nape.

Waziri huyo pia alitoa tahadhari kwa wazazi, walezi na walimu wanaowapa watoto vishkwambi kwa lengo la kujifunza, kuwa makini kwa kuwa ndivyo vinatumika kutazamia maudhui yasiyo na maadili kwa makuzi yao.

Kuhusu usalama wa anga la mtandao, alisema lipo salama na TCRA inaendelea kufanya kazi kuhakikisha linaendelea kuwa salama.

Nape alisema serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu wasambazaji wa maudhui yasiyozingatia maadili ya Mtanzania ikiwa ni pamoja na yale yenye viashiria vya ushoga na usagaji.

Aliahidi pia wataendelea kuweka mkazo na uhamasishaji wa utengenezaji wa maudhui ya ndani yenye ubora na yanayozingatia utamaduni, mila, desturi na maadili ya Mtanzania.

# Mifuko ya plastiki yageuka kitendawili

**Na Jenifer Gilla**

LICHA ya serikali kupiga marufuku matumizi ya vifungashio vya plastiki visivyokidhi vigezo, bidhaa hiyo inauzwa kinyemela na kutumika kwenye masoko na maduka. Imebainika.

Agosti 25, mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, alitoa agizo kwa niaba ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, kuwataka watendaji wote kufuatilia na kuondoa bidhaa hiyo ambayo ni tishio kwa uharibifu wa mazingira.

Pia aliliagiza Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), kuanzisha operesheni ya kutokomeza vifungashio hivyo mara moja na kuwachukulia hatua wanaokaidi agizo hilo.

Uchunguzi wa Nipashe kwenye baadhi ya masoko na maduka umebaini wafanyabiashara wakiendelea kuuza bidhaa hiyo kwa bei ya jumla huku wachuuzi wa mboga wakiitumia kubebea bidhaa zao.

Tangazo la Halmashauri kutisisha matumizi ya mifuko hiyo, limebandikwa katika masoko ya Dar es Salaam.

Mmoja wa wafanyabiashara aliyekutwa akiuza mifuko hiyo ambaye hakutaja kutaja jina lake, alisema analazimika kuiuza ili asipate hasara kwa sababu aliinunua mingi na bado haijaisha.

"Tangazo nimeliona na maagizo ya jiji nimeyasikia dada yangu, lakini siwezi kuacha kuiuza kwa sababu hii yote ni pesa dada, nikiipeleka kwa ofisi kama tulivyoambiwa ina maana nitapata hasara, nitaiuza mpaka iishe ili nirudishe pesa yangu," alisema mfanyabiashara huyo.

Muuza nyama ya ng'ombe soko la Temeke, Ahmedi Ally, alisema anatumia vifuko hiyo kwa sababu wateja wanaokwenda kununua kitowewo hicho hawabebi mifuko, na wengi hufuata mahali wanapopewa mifuko.

"Inabidi wateja nao waelimishwe kwa sababu hawaji na mifuko, wakikukuta hauna mifuko wanahama wanakwenda kwa mwenzako, na mimi hapa natafuta chochote inabidi niwe nayo ili nisikose kuuzia wateja," alisema.

Naye muuza mboga soko la Tabata, Amina Salim, alisema baadhi ya wafanyabiashara kuendelea kutumia bidhaa hizo wakati zimeshapigwa marufuku ni kinyume na agizo la serikali.

Alisema alikuwa akitumia bidhaa hiyo, lakini aliiacha baada ya kuelimishwa madhara yake na viongozi wa masoko na kuwataka wafanyabiashara wenzie kutii agizo la serikali.

"Hawa wateja ni sisi wenyewe ndiyo tunawazoesha vibaya, hapa tukiamua wote kwa kauli moja tusiweke hivi vifungashio wateja watakuja na mifuko yao, mbona wapo wanaokuja na mifuko yao tangu lile katazo la kwanza. Wakija hapa na kuona wengine wanatoa hiyo mifuko wanazoea vibaya," alisema Amina.

**MADHARA YA PLASTIKI**

Akizungumza na ITV, Septemba 7, mwaka huu, Meneja wa Kanda ya Mashariki kutoka Baraza la Taifa Usimamizi wa Mzingira (NEMC), Anord Mapinduzi, alisema mifuko hiyo imezuiwa kutumika kutokana na matumizi kuwa makubwa na usimamizi duni unaowezesha kuingia kwenye mazingira na kusababisha madhara.

"Plastiki inavyopata joto au unavyoichoma unaharibu ile fomula yake, inaanza kuvunjika inaachia, inavyoachia inaruhusu viambata sumu kutoka na kuingia kwenye vitu ambavyo tunavitumia ambavyo huingia mwilini mwetu kupitia vyakula au vinywaji au kwa kuvuta hewa na kutuathiri kidogo kidogo, baada ya miaka mingi unakuta mtu amepata kansa," alisema Mapinduzi.

Pia viambata sumu katika mifuko hiyo vinaweza kuathiri mfumo wa uzazi na kusababisha kuzaliwa watoto wenye tatizo. Kadhalika inachangia kwa kiasi kikubwa kutokea kwa mafuriko hata inaponyesha mvua ndogo kwa sababu hujazana kwenye mitaro na mifumo ya majitaka na kuziba.

"Mpaka juzi tulikuwa tumeshakusanya tani 43 (za mifuko ya plastiki) kwa Dar es Salaam na tunategemea na mikoa mingine inaendelea. Wameelekezwa (wafanyabiashara) wasalimishe mifuko hiyo, wale wa sokoni wasalimishe mifuko hiyo hapo hapo, wengine wapeleke serikali ya mitaa na halmashauri itazikusanya halafu Baraza (NEMC) itaweka utaratibu wa kuzikusanya kwenye halmashauri kwa ajili ya uteketezaji.

**CHANGAMOTO YA UTEKELEZAJI**

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema baadhi ya changamoto wanazokutana nazo katika kutokomeza mifuko hiyo ni njia za panya za uingizaji wa mifuko hiyo, pia ushirikiano mdogo serikali za mitaa.

Machi 8, mwaka jana NEMC ilitangaza faini kwa watumiaji wa vifungashio ambavyo havikidhi vigezo kuwa ni kuanzia Sh. 30,000 hadi Sh. 500,000 na wasambazaji hadi Sh. milioni 10 au kifungo cha miaka mitatu hadi saba, huku wazalishaji na waingizaji ni Shilingi milioni tano hadi 10.

Aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, January Makamba, Mei 17, mwaka 2019 alisaini kanuni ya mazingira ya kukataza matumizi ya mifuko ya plastiki, uzalishaji, uingizaji, uhifadhi, usambazaji au utumiaji, ambazo zilianza kutumika Juni mosi, mwaka huo.


SIMU: 0785 944141
0766 547725

TANFIN CONSULTANT

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA/NOTISI

**TANFIN CONSULTANT E.A. LTD** kwa niaba ya **SHREE HINDU MANDAL SACCOS LTD,** tunatoa notisi na Tangazo kwa wadaiwa/Wadhamini wafuatao wawe wamelipa madeni yao wanayodaiwa na **SHREE HINDU MANDAL SACCOS LTD.** Kinyume na hapo tutauza dhamana/Mali za wadaiwa/Wadhamini hao kwa njia ya mnada wa hadhara. Mnada utafanyika sehemu dhamana/mali husika ilipo kuanzia saa nne asubuhi na kuendelea na kwa tarehe kama ilivotangazwa hapo chini.

| S/N | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | AINA YA DHAMANA ITAKAYOUZWA NA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | REHEMA TIJANI MZEE | NYUMBA NA ENEO LILILOPO NA ENEO LA KUPIGA TOFALI, DEGE-KATA YA SOMANGIRA – KIGAMBONI ENEO LILILOPIMWA KITUNDA, WILAYA YA ILALA | 11/10/2022 |
| 2. | HELLEN ANSWEPA KAYORA | NYUMBA- ILIOPO MTAA WA MALELA, KATA YA TOANGOMA, WILAYA YA TEMEKE. | 12/10/2022 |
| 3. | LINJE JAMES MTELELAH | KIWANJA-AMANA KATA YA MAKANGARAWE, WILAYA YA TEMEKE. | 13/10/2022 |
| 4. | MWANAISHA ABDALLAH MLOKA | NYUMBA-MTAA WA MAKANYA-TANDALE WILAYA YA KINONDONI | 18/10/2022 |
| 5. | UPENDO KAPOGO | NYUMBA ILIYOPO MAVURUNZA – BONYOKWA, KIMARA, WILAYA YA UBUNGO. | 20/10/2022 |
| 6. | DISMAS STEPHENO HOMANGA | KIWANJA – LESENI O. ILA026442 KIWANJA No. ILA/UKG/MZZ21/113; MTAA WA MAZIZINI; KATA YA UKONGA- WILAYA YA ILALA. | 21/10/2022 |
| 7. | ELIZABETH ADOLPH JOHN | MASHAMBA YALIYOPO KISARAWE II, WILAYA YA KIGAMBONI. | 22/10/2022 |
| 8. | HERRIETH MWAKIFULEFULE | KIWANJA PLOT NAMBA 457 BLOCK A MTAA WA KIEGEYA A KATA YA KIEGEA MANISPAA YA MOROGORO | 26/10/2022 |

**MASHARTI YA MNADA**

1. MNADA utafanyika sehemu dhamana ilipo na zitauzwa kama zilivyo.
2. MNUNUZI atakaeshinda atalazimika kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya bei iliyofikiwa papohapo na asilimia sabini na tano (75%) atalazimika kulipia ndani ya siku kumi na nne 14 kuanzia tarehe ya MNADA.
   Endapo mteja atashindwa kumaliza asilimia sabini na tano(75%) ndani ya siku 14 kiasi kilicholipwa awali 25% hakitarudishwa na MNADA utarudiwa tena.
3. Gharama za kubadilisha umiliki ( Transfer of ownership) pamoja na gharama nyingine zinazohusiana na umiliki wa mali hizi ni juu ya MNUNUZI.



**MWAMBA MILLENIUM COURT BROKER AND CO LTD**

## MNADA WA HADHARA

KWA AMRI YA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA KONDOA TUTAENDESHA MNADA WA HADHARA WA KUUZA NYUMBA ILIYOPO KATA YA SONGOLO KIJIJI CHA SONGOLO WILAYA YA CHEMBA. MALI YA NDUGU HALFAN RAMADHAN NDWATA ILI KUFIDIA DENI ANALODAIWA NA NDUGU ATHUMANI NKUNDULO. MNADA UTAFANYIKA TAREHE 16/09/2022 SAA TANO KAMILI ASUBUHI (5:00)

**MASHARTI YA MNADA**

- UKAGUZI UNARUHUSIWA KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI
- MALIPO 25% BEI ITAKAYOWEKWA KWENYE MNADA NA 75% ATAMALIZIA NDANI YA SIKU 14
- ENDAPO MNUNUZI ATASHINDWA KULIPA SALIO KWA MUDA ULIOWEKWA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI ZOTE
- KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA KWA SIMU NAMBA 071224577/ 0756364501

**WOTE MNAKARIBISHWA**



**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**

**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NA 174 YA MWAKA 2022.**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**KISUSE KALIP MWANYOMBOLE**

**MATILDA MWANYOMBOLE.....................MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 04 mwezi wa October, 2022.

Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 1 mwezi wa Septemba, 2022.

HIGH COURT OF TANZANIA

NAIBU MSAJILI



**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**ONE STOP JUDICIAL CENTRE OF TEMEKE**
**AT TEMEKE**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE PAUL FREDERICK GATRELL**
**AND**
**IN THE MATTER OF NOTIFICATION TO CREDITORS BY THE APPOINTED ADMINISTRATRIXES**
**HELLEN DE VERE VAN DER LINDEN AND CLARE LINA PITMAN**

**NOTICE TO CREDITORS**
**(Rule 111)**

NOTICE is hereby given that all persons claiming debts or liabilities affecting the estate of the above named Paul Fredrick Gatrell deceased, who died at Blantyre Adventist Hospital in Malawi on the 15th day of September 2017 and probate of whose letters of administration were granted to us by the High Court of Malawi (Principal Registry) on the 5th day of April 2018 and re-sealed by the High Court of Tanzania (Temeke High Court sub-registry: One Stop Judicial Centre) on 10th May, 2022 are hereby required to send in their claims to us at the following address within thirty days from the date of publication of this notice at the expiration of which time we shall proceed to hand over the assets to the persons entitled thereto having regard only to the claims which we shall then have had notice.

**HELLEN DE VERE VAN DER LINDEN & CLARE LINA PITMAN**

**HOUSE NO. 76, CHOLE ROAD,**
**MASAKI,**
**P.O. Box 23490**
**DAR ES SALAAM.**

# Amchinja mpenzi wake naye ajikata koromeo

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKULIMA wa Kijiji cha Mshikamano, Wilaya ya Nachingwea, Albert Mkuwele (49), amemuua kwa kumchinja kwa panga mpenzi wake, Rejina Sotti (46) kisha naye kujiua kwa kujikata koromeo.

Taarifa zilizopatikana kutoka kijijini hapo na kuthibitishwa na viongozi na watendaji wa serikali wa kata hiyo, zinaeleza Mkuwele alitekeleza unyama huo, Septemba 9, mwaka huu.

Diwani wa Kata ya Mitumbati, Saimon Njende na Ofisa Mtendaji, Emmanuel Ndunguru, walisema wapenzi hao waliishi pamoja kama mke na mume kwa miaka 28 na kubahatika kupata watoto wanne na wajukuu wawili.

Alisema kabla ya mauaji hayo, wapenzi hao walionekana kutokuwa na maelewano mazuri kwa muda mrefu hali iliyomsukuma Mkuwele kuondoka na kwenda kuishi kijiji kingine.

"Wapenzi hawa hadi wanauana hawakuwahi kufunga ndoa na wameishi pamoja kwa miaka 28, wamebahatika kupata watoto wanne na wajukuu wawili," alisema Diwani Njende.

Alisema siku ya tukio, mwanaume alirejea nyumbani na kuwakuta watoto alipowauliza alipo mama yao na kujibiwa kuwa yupo shambani akivuna mbaazi, alionekana akichukua panga huku akilinoa na kuelekea alipo mpenzi wake ambako alitekeleza mauaji hayo.

Taarifa zinasema kuwa alimkata shingo na kutenganisha kichwa na kiwiliwili, baadaye kugeuza panga alilolitumia kumjichinjia mzazi mwenzake, kujikata koromeo na kufariki papo hapo.

Mtendaji Kata ya Mitumbati, Emmanuel Ndunguru, alisema alipopata taarifa hizo, aliitaarifu Polisi ambao walimchukua daktari kutoka Hospitali Wilaya ya Nachingwea kwenda eneo la tukio kwa ajili ya uchunguzi wa miili hiyo.

Alisema baada ya uchunguzi wa kitaalamu, waliruhusu ndugu kuendelea na taratibu za mazishi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, ACP Pili Mande, alipoulizwa kuhusu tukio hilo, alisema taarifa hiyo haijamfikia mezani kwake na kuahidi kuifuatilia.



Mkuu wa Dawati la Elimu kwa Umma wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kinondoni, Bibie Msumi (kushoto) na viongozi wengine wakipata maelezo kwa Katibu wa Shirika la Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Samaha Semanga, kuhusu shirika hilo linavyofanya kampeni ya kupambana na rushwa ya ngono kwa wanafunzi kwa kutumia njia mbalimbali, ikiwamo vipeperushi, Mwananyamala Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Waziri Gwajima: Fursa zilizoko zitumike kuondoa ombaomba

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amesema ipo haja ya majukwaa ya uwezeshaji kiuchumi kutumika kufikisha elimu kwa wananchi walioko vijijini ili watumie fursa zilizoko kuondokana na kukaa barabarani kuomba msaada.

Dk. Gwajima alitoa rai hiyo jana alipozindua Mwongozo wa Kitaifa wa Uanzishaji na Uendeshaji Majukwaa ya Uwezeshaji Kiuchumi uliofanyika Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Julius Nyerere kilichoko Kwamfipa, Kibaha.

Alisema kuna haja ya wataalamu katika idara zinazohusika na majukwaa ya kuchumi, kuwafikia wananchi walioko vijijini na kuwapa elimu ya namna ya kutumia fursa zilizopo na kukuza vipato vyao na jinsi ya kupata mikopo inayotolewa na halmashauri.

Majukwaa ya uwezeshaji kiuchumi ni mlango wa kufanya mapinduzi ya kumfanya mwanamke ainuke kiuchumi, hivyo kuwapo kwa elimu ya kutumia fursa itawafanya wanawake kuwa na mabadiliko na kuacha utegemezi.

"Lazima tufike kwenye mitaa na vijiji, shehia na kata kwa lengo kila mwanamke atumie fursa zilizoko badala ya kuonekana barabarani akihitaji kusaidiwa wakati kuna fursa nyingi," alihimiza.

Akizindua mwongozo huo kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, waziri huyo alisema wataalamu wanaohusika, wanatakiwa kujikita vijijini badala ya kuelimisha walioko ofisini ambao wanafahamu kila kitu kuhusiana na fursa na sheria zilizopo.

Awali akimkaribisha waziri huyo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mkuu wa Wikaya ya Kibaha, Sara Msafiri, alisema mkoa huo umeanzisha majukwaa 1,722 na zaidi ya 900 yamesajiliwa.

Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Zainabu Chaula, alisema mwongozo huo utakuwa kichocheo cha ukuaji wa wanawake kiuchumi.

Chaula pia aliwataka wanawake kulitumia Shirika la Posta kutangaza bidhaa zao nje ya nchi.

Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Mariam Abdallah, alisema wataendelea kutekeleza mwongozo huo kuhakikisha maendeleo kwa wanawake yanapatikana.

Katibu Mtendaji Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Bengi Issa, alibainisha kuwa hadi kufikia Juni mwaka huu, majukwaa 26 kwenye ngazi ya mkoa yalianzishwa, ngazi ya kata majukwaa 1,354 na vijiji/mitaa majukwaa 1,859.

Alisema majukwaa hayo yamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali, maandiko ya kibiashara na yamenufaika na fursa mbalimbali zilizojitokeza.

Mwakilishi wa Shirika la Legal Services Facility (LSF), Deogratius Bwire, alisema kwa kupindi cha miezi sita iliyopita, wamefanikisha kutoa msaada wa kisheria kwa wanawake wenye vikwazo vya kiuchumi 789.

Bwire alisema tayari wanawake hao wamepata mali zao yakiwamo mashamba na viwanja.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake Mkoa wa Pwani, Mariam Ulega, alisema asilimia 50 ya majukwaa yaliyoanzishwa katika mkoa huo yamesajiliwa na wataendelea kuyalinda na kuyaendeleza kufikia malengo yake.

# Polisi yadai kunasa mirungi tangi la mafuta

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi mkoani Arusha limewakamata watu 38 kwa tuhuma za kujihusisha na matukio mbalimbali ya kihalifu huku mmoja wao akidaiwa kusafirisha dawa za kulevya aina ya mirungi kwa kuzifichwa ndani ya tangi la lori la mafuta.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi wa Polisi Justine Masejo, alibainisha hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari, akisema watuhumiwa hao walikamatwa kwa nyakati tofauti katika operesheni iliyofanyika kuanzia Septemba 5 hadi 10 mwaka huu.

Alisema operesheni hiyo iliongozwa na Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Mkoa huo kwa lengo la kuwasaka watuhumiwa wa uhalifu.

Alibainisha kuwa Septemba 10 majira ya saa 12:30 asubuhi, katika Mtaa wa Kikwe, Kata ya Kikwe wilayani Arumeru, jeshi hilo lilifanikiwa kumkamata Allen Kasamu (49), dereva na mkazi wa Suye jijini Arusha, akiwa anasafirisha dawa za kulevya aina ya mirungi yenye uzito wa Kg 390.75.

"Mtuhumiwa huyo alikamatwa akiwa anasafirisha dawa hizo za kulevya kwa kutumia gari aina ya Mitsubish Canter Tanker, ambalo ni maalum kwa ajili ya kubeba mafuta ambapo alitumia mbinu za kupakia ndani ya tangi la mafuta ili asijulikane," alisema Masejo.

Aliongeza kuwa katika operesheni hiyo, pia walifanikiwa kukamata pikipiki 13 zilizokuwa zinatumika katika matukio ya uhalifu, pombe aina ya gongo lita nane, bangi yenye uzito wa kilo 70 na kompyuta mpakato tatu.

Kamanda Masejo alisema Jeshi la Polisi mkoani Arusha linaendelea na upelelezi na kuwahoji watuhumiwa hao na pindi upelelezi ukikamilika, jalada litapelekwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

Alitoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu kwa jeshi hilo ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga jipangeni CAF kwa 90 zingine, kazi haijaisha

**WAWAKILISHI** wa Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba na Yanga kwa upande wa Tanzania Bara, wameanza vizuri mechi zao za raundi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini huzuni kubwa ni kwa Tanzania Visiwani kutokana na KMKM kuanza kwa kuangukia pua nyumbani.

Simba ikiwa ugenini nchini Malawi juzi, iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya wenyeji wao, Nyasa Big Bullets, wakati Yanga ambayo kikanuni nayo ilikuwa ugenini licha ya mchezo wao dhidi ya Zalan FC kupigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, ilitoka na ushindi mnono wa mabao 4-0.

Zalan FC ya Sudan Kusini, iliutumia Uwanja wa Benjamin Mkapa kama wao wa nyumbani kutokana na hali ya usalama nchini kwao kutokuwa shwari, hivyo mechi ya marudiano Jumamosi wiki hii, itapigwa tena uwanjani hapo Yanga sasa ikiwa mwenyeji.

Balaa kubwa siku hiyo kwa wawakilishi wengine wa nchi kwa upande wa Tanzania Visiwani, timu ya KMKM, ilikubali kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa Al Ahli Tripoli ya Libya, hivyo mchezo wa marudiano itakuwa na mlima mrefu wa kubadili matokeo hayo ili kusonga mbele.

Hata hivyo, bado tunaamini hakuna kinachoshindikana ndani ya dakika 90, kwani kama Al Ahli Tripoli iliweza kuibuka na ushindi huo ugenini, pia KMKM inaweza 'kupindua meza' nchini Libya kama ikijipanga vizuri na kurekebisha ilipokosea, kwa kuwa tayari inamjua vema mpinzani wake.

Lakini pia katika hilo, kwa Simba na Yanga, hazipaswi kubweteka kwa matokeo mazuri ziliyopata kwani tulishawahi kushuhudia wapinzani wao wakija hapa nchini na kupindua meza kutokana na wenyeji kuamini tayari wameshamaliza mchezo.

Hilo linatufanya kuwaonya wawakilishi wetu hasa tukikumbuka Agosti 10, 2019, wakati Simba ilipotoka sare tasa ugenini dhidi ya UD Songo ya Msumbiji na katika mechi ya marudiano Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam wakati huo Luis Miquissone akiichezea UD Songo, akaipatia bao la kuongoza dakika 12, lililodumu hadi dakika ya 87 Erasto Nyoni aliposawazisha kwa mkuju wa penalti, hivyo kuwafanya wageni hao kusonga mbele kutokana na faida ya bao la ugenini, safari ya Simba ikiishia hapo.

Kadhalika, Oktoba 17, mwaka jana katika michuano hiyo, Simba iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 ugenini dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana na kurejea nchini kifua mbele ikiamini imemaliza mchezo na wanachokisubiri ni kukamilisha ratiba tu kabla ya kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo.

Kilichowakuta katika mchezo wa marudiano Oktoba 24, 2021, hakuna aliyeamini baada ya mashabiki, wachezaji, benchi la ufundi na uongozi wa klabu hiyo kutoka Uwanja wa Benjamin Mkapa vichwa chini kutokana na kukubali kichapo cha mabao 3-1, hivyo kuangukia kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Mifano hiyo hai ya hivi karibuni, ndiyo inayotufanya kuzionya Simba na Yanga, tukizitaka kuchukua tahadhari mapema kwa kuingia uwanjani katika mechi za marudiano zikiamini bado mchezo haujaisha hadi dakika 90 za pili zitakapomalizika wakiongoza kwa jumla ya mabao ya nyumbani na ugenini.

Pamoja na mtaji mkubwa kwa Yanga ilionao wa mabao 4-0, na ule wa Simba wa magoli 2-0, bado haitoshi kuwa sababu ya kubweteka katika mechi za marudiano, kwani katika mchezo wa soka ukifanya makosa tu unaadhibiwa jambo ambalo linaweza kutokea wakati wawote kama wachezaji hawatajengwa kisaikolojia kwa kujazwa ari ya kupambana mwanzo mwisho.

Sisi tunatamani kuona Tanzania kwa mara ya kwanza inaweka rekodi ya kuingiza timu zote tatu; Simba, Yanga na KMKM katika hatua ya makundi na hilo linawezekana tu kama kila mmoja kuanzia mashabiki, wachezaji, benchi la ufundi na viongozi watatimiza wajibu wao nje na ndani ya uwanja.

Tunaamini mabenchi ya ufundi ya wawakilishi wetu hao kimataifa, wameona ulipo ubora na udhaifu wa wapinzani wao kama ambavyo nao tayari wamewaona, hivyo kinachotakiwa ni kufanya kazi ya ziada kwa siku hizi sita zilizobaki kabla ya mechi za marudiano.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba msitumie mechi za kimataifa kujaribu wachezaji

**KWENYE** mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC, wanachama na mashabiki wa Simba walichachamaa na kucharuka, wakitaka Kocha Msaidizi Selemani Matola ajiuzulu kwa madai kuwa hawana imani naye.

Hapa naomba nieleweke, nilivyowasikia na kuwasoma wanachama na mashabiki wa timu hiyo siyo kwamba Matola si kocha mzuri, la hasha, ila hawana imani naye.

Hali ilikuwa mbaya kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa baada ya timu hiyo kulazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya KMC kwenye mechi ambayo wachezaji walicheza kana kwamba walishacheza soka miaka mingi iliyopita na wamestaafu na hiyo ilikuwa ni bonanza wakijikumbushia enzi zao tu.

Hakuwakuwa na ari, nguvu, kasi, wala kitu chochote kile ambacho kinaweza kukupa picha kama wanaoonekana uwanjani ni wachezaji wa Ligi Kuu Tanzania Bara, tena wa timu kubwa kama Simba.

Ndiyo maana wengi walikata tamaa hata kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Nyasa Big Bullets kama timu itafanya vizuri.

Labda kwa kuliona hilo na mengineyo, viongozi wa Simba wakamchukua kocha mkongwe Juma Mgunda kuchukua kijiti hicho kwani ilikuwa ni siku chache baada ya klabu hiyo kuachana na kocha wake, Zoran Maki.

Hiki ni kipindi kigumu na cha mpito kwa klabu hiyo, kwani Mgunda ni kocha wa muda wakati ikisaka kocha mwingine atakayekuja kuwa kocha mkuu.

Mimi si mtabiri, lakini nadhani atakapokuja kocha, Mgunda ana nafasi kubwa ya kuwa kocha msaidizi kwenye kikosi hicho.

Kama alivyowahi kusema Kocha wa sasa wa Al Hilal ya Sudan, Florent Ibenge kuwa linapokuja suala la mechi za Ligi ya Mabingwa, Simba inakuwa ni timu nyingine kabisa na si ile inayoonekana kwenye Ligi Kuu.

Alisema ukiipeleleza Simba ili kujua jinsi gani ya kuidhibiti tafuta video zake za mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho ili ukabiliane nayo, lakini ukichukua za Ligi Kuu itakula kwako, kwani haipo kama vile inavyokuwa kimataifa. Kwenye Ligi Kuu inacheza kawaida, sana lakini ikiwa kimataifa inabadilika na kuwa timu ya kutisha.

Na ndivyo ilivyokuwa, kwani ikiwa ugenini nchini Malawi ilishinda mabao 2-0.

Nilichokiona ndicho kilichonifanya niandike hili. Baada ya mechi dhidi ya KMC, baadhi ya madai ya mashabiki ni kwamba kwa sasa kwa sababu Matola ana nguvu baada ya Zoran kuondoka, basi tutaona baadhi ya wachezaji ambao hawajacheza hata siku moja wanacheza. Tunaona hata wachezaji ambao hawako fiti sasa watacheza.

Nikajua tu ni wale ambao wanaongea tu bila kujua wanachokisema, au wanafuata mkumbo, lakini kwenye mechi dhidi ya Nyasa Big Bullets nikamkumbuka shabiki yule.

Moja ya mabadiliko ambayo yaliiumiza Simba na kusababisha kushambuliwa sana kipindi cha pili ni kuingia kwa Erasto Nyoni baada ya kutoka Sadio Kanoute. Ilinishangaza. Hata wale tuliokuwa nao tunaangalia mpira kabla hata hawajaingia walianza kuwa na wasiwasi na mabadiliko hayo, pamoja na ya John Bocco.

Kilichotokea ni kile kile ambacho watu walikuwa na wasiwasi nacho. Hakuna chochote alichofanya Nyoni kwenye mechi hiyo. Hakuonekana kwenye tukio lolote muhimu zaidi ya kukimbia kivivu uwanjani, kuchukua mpira na kutoa pasi. Aliingia kama kiungo mkabaji, lakini hakukaba mtu yeyote. Kazi ya ziada sasa ilifanywa na Mzamiru Yassin aliyeanza mechi tangu mwanzo alikuwa uwanjani muda wote lakini alionekana kufanya vema kuliko aliyeingia kumsaidia.

Kwa bahati nzuri Bocco alifunga bao kwa msaada mkubwa wa Clatous Chama, lakini ukiondoa hilo hakuwa na madhara sana.

Naweza kusema kuingia kwa Nyoni kuliwafanya wenyeji kupata mwanya wa kulishambulia lango la Simba kama nyuki, kiasi cha kuwafanya kina Mohamed Ouattara, Henock Inonga ambaye aliacha kabisa masihara yake kwenye mechi hiyo, Israel Mwenda aliyekuwa kwenye kiwango cha juu, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' na kipa wao Aishi Manula kufanya kazi kubwa kuzuia hatari zote.

Hapa kuna swali. Unamtoaje Kanoute ambaye alikuwa mchezoni vilivyo huku akiwa hana hata kadi ya njano na kumwingiza Nyoni asiye na kasi na hana asili ya kiungo mkabaji mpambanaji kwenye mechi kama hiyo ya ugenini na timu imezidiwa? Nyoni ambaye hakucheza mechi yoyote hata ya ligi akaingizwa kwenye mechi ya kimataifa ngumu kama ile?

Ukweli ni kwamba kuwaingia wachezaji ambao hawajacheza hata mechi za Ligi Kuu kwa dakika 90 mechi za kimataifa ni hatari na ni kama kujitoa muhanga.



Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Patrick Kasango (wa tatu kushoto), akifungua mkutano wa kupata maoni ya wanawake wenye ulemavu Tanzania. Mkutano huo ulifanyika ukumbi wa Katala Beich mjini Singida juzi.Wa pili kushoto ni Mkurugenzi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Sheed Mafta na wa nne kushoto ni Mratibu wa Mradi Kitengo cha Ushiriki wa Wanawake kwenye Uongozi wa Siasa (UN-Women), Erasmina Massawe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC Telak aamuru mwalimu aliyetimuliwa kazi kurejeshwa

**Na Said Hamdani**, LINDI

MKUU wa Mkoa wa Lindi, Zainabu Telak, ameamuru kurejeshwa kazini mwalimu wa Shule ya Msingi Mtende, Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, Stanley Ngaiza, aliyefukuzwa kwa madai ya utoro.

Telak alitoa agizo hilo, wakati wa kikao cha elimu kilichofanyika Manispaa ya Lindi.

Alitoa amri hiyo baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Katibu wa Chama cha Walimu (CWT) Wilaya ya Kilwa, Hamisi Bakari, kutimuliwa kazi mwalimu huyo kwa utoro wa siku 11 kwa kosa linalodaiwa la kubambikiwa na uongozi wa Tume ya Walimu (TSC) Wilaya ya Kilwa.

Mwalimu Ngaiza alifukuzwa kazi mwezi Aprili, mwaka huu na kukata rufani mamlaka ya juu mkoani Dodoma kupinga uamuzi huo.

Akitoa amri hiyo, Mkuu huyo wa mkoa alisema, kitendo cha mwalimu huyo kufukuzwa kazi kwa kosa lisilo lake ni uonevu na kuamuru arejeshwe mara moja kazini, aweze kuendelea kutekeleza majukumu yake ya kufundisha watoto.

"Viongozi acheni kuonea watumishi mliopewa kuwaongoza, Lindi tuna upungufu wa watumishi, mnafukuzaje kazi kwa kosa lisilo lake?" Alihoji Telak.

Alisema amekuwa akipokea malalamiko mengi kutoka kwa watumishi walio chini yao, yanayodai unyanyasaji unaofanywa na baadhi ya viongozi, huku akiwataka kujirekebisha na kuonya vyeo walivyonavyo ni dhamana na sio silaha za kuonea wenzao.

Mwanzoni akiwasilisha malalamiko hayo, Katibu wa CWT Wilaya ya Kilwa, Hamisi Bakari, alishauri kwenye kikao hicho, kabla TSC haijachukua uamuzi wa kufukuza kazi walimu ni vizuri wakakaa pamoja kuangalia tatizo.

# NRA kuchagua viongozi Sept 24

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha National Reconstruction Alliance (NRA), kinatarajia kufanya uchaguzi wa viongozi wake wa kitaifa Septemba 24, mwaka huu, mkoani Morogoro.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mwenyekiti wa Uchaguzi wa chama hicho Taifa, Leopold Mahona, alisema uchaguzi huo utafanyika katika mkutano wake mkuu.

Mahona alisema katika kufikia huko tayari chama hicho kimetoa ratiba ya mchakato mzima wa uchukuaji na urejeshaji wa fomu kwa wagombea.

"Kabla ya kufikia siku ya uchaguzi mkuu utakaofanyika Septemba 24, mwaka huu, kwenye mkutano mkuu wa chama tumetoa ratiba ya mwelekeo wa kazi hiyo ikiwa ni takwa la kikatiba na sheria ya chama," alisema Mahona.

Alisema dirisha la uchukuaji na urejeshaji wa fomu hizo ulianza Septemba 8, mwaka huu na unatarajiwa kufungwa Septemba 14, mwaka huu.

"Na Septemba 14 ndiyo itakuwa siku ya uteuzi wa wagombea na siku tatu baada ya hapo zitakuwa za kupokea na kushughulikia pingamizi na Septemba 21 hadi 23 itakuwa ni kipindi cha wagombea kufanya kampeni," alisema Mahona.

Alitaja nafasi zinazogombewa kuwa ni ya Mwenyekiti Taifa na Makamu Wenyeviti Tanzania Bara na Zanzibar.

Nafasi nyingine ni Katibu Mkuu, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini na Katibu wake pamoja na Mwenyekiti wa Baraza la Wazee na Katibu wake.

"Na katika hili tunawasisitiza wanachama wetu kujitokeza kwa wingi kuchukua fomu za kuwania nafasi hizo za kitaifa. Tunaomba pia wanawake na makundi mengine wasibaki nyuma," alisema Mahona.

Miongoni mwa sifa kuu za wagombea ni kuwa mwanachama hai wa chama hicho, kujua kusoma na kuandika, kielelezo cha maendeleo na wanatakiwa kuwa na umri wa miaka 18 na kuendelea.

# MISA Tanzania yasisitiza umuhimu mabadiliko ya sheria wanahabari

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Jangwa la Sahara, Tawi la Tanzania (MISA-Tanzania), imesema kuna ulazima wa kufanya marekebisho ya sheria zinazosimamia taaluma ya uandishi wa habari na utangazaji nchini kwa haraka kwa maendeleo ya nchi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa ripoti ya ripoti ya mwenendo wa vyombo vya habari nchini ya mwaka 2015 hadi 2020 na 2021, iliyoangazia sheria zinazosimamia taaluma hiyo kwa Tanzania Bara na Visiwani.

Pia ripoti hiyo inapendekeza na kumwomba Rais Samia Suluhu Hassan kutoa tamko ambalo litasaidia kuharakisha marekebisho ya sheria zenye ukakasi katika tasnia hiyo.

Kadhakila, inaliomba Bunge kutoa kipaumbele kwenye marekebisho ya sheria zinazolalamikiwa na wadau kwa kuwa zinakwaza taaluma ya uandishi wa habari nchini.

Sheria hizo ni ya Huduma za Vyombo vya Habari mwaka 2016, Sheria ya Takwimu na Sheria ya Udhibiti wa Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (EPOCA).

"Rais akisimama kama Mkuu wa nchi na kuzungumzia kuhusiana na sekta ya habari, basi hata watendaji wake inakuwa ni rahisi kufanyia kazi kwa haraka marekebisho ya sheria hizo zenye ukakasi katika tasnia ya habari," alieleza mmoja wa waandaaji wa ripoti hiyo, Edwin Soko na kuongeza:

"Kwenye hii ripoti sehemu kubwa sana ya 'findings' (matokeo) asilimia 80 ya tuliowahoji walisema kwamba uhuru wa vyombo vya habari kuanzia mwaka 2015 hadi 2020 uliporomoka na pia walisema sheria tulizokuwa nazo hazikuwa rafiki."

Makamu Mwenyekiti wa MISA-Tanzania, James Malenga, alisema mengine yaliyoangaziwa katika ripoti hiyo ni madhira wanayokutana nayo waandishi wa habari na mazingira ya kufanyia kazi kwa ujumla.

Miongoni mwa vitu alivyovitaja kubainishwa katika ripoti hiyo ni changamoto ya kisheria hususani Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari 2016 na Sheria Makosa ya Mtandao 2016 na kwamba kilio kikubwa cha wadau katika tasnia hiyo ni kuona marekebisho yake yanafanyika kwa uharaka.

"Mathalani, Sheria ya Huduma za Habari kuna baadhi ya changamoto ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho, kwa mfano kipengele kinachompa waziri husika mamlaka ya kufungia vyombo vya habari, hiki nacho ni kilio kikubwa kwa wanatasnia kifanyiwe marekebisho," alisema Malenga.

Meneja wa Programu wa Taasisi ya Kimataifa inayosaidia Vyombo vya Habari (IMS), Fausta Musokwa, alisema ripoti hiyo ni muhimu kwa kuwa inaongeza uelewa kwa wadau wa tasnia hiyo kuhusu uboreshaji wa sheria za habari ili zihamasishe uhuru wa kujieleza na kutoa taarifa.

Mwanasheria aliyekuwa miongoni mwa waandishi wa ripoti hiyo, Swedy Shilinde, alisema mambo mengine yaliyoainishwa kwenye ripoti hiyo ni namna Jeshi la Polisi linavyotumia nguvu kuwachukulia hatua waandishi wa habari.

"Katika ripoti hii, moja ya vitu ambavyo tumebaini ni namna ambavyo Jeshi la Polisi limekuwa likiwashughulikia waandishi wa habari wanapotuhumiwa. Kumekuwa na makosa mengi sana ambayo yanafanywa pale mwandishi wa habari au mlaji wa taarifa za mitandaoni anapokutwa na madhira," alisema Swedi.

"Namna wanavyoshughulikiwa ni tofauti na wengine, waandishi wa habari wengi wanapokamatwa namna wanavyoshughulikiwa kwenye vituo vya polisi mpaka kufikia mahakamani inaleta shida kidogo.

Wengine wanachukuliwa utafikiri tayari ni wahalifu moja kwa moja, wanatakiwa wachukuliwe kama watuhumiwa mpaka pale mahakama inapoamua."

# Waziri atoa somo kwa wafugaji kufuga kisasa

**Na Beatrice Shayo**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amewashauri wafugaji kununua ardhi kwa ajili ya ufugaji wa kisasa na kuweka miundombinu muhimu ili kukuza uchumi wao na taifa kwa ujumla.

Kiongozi huyo aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipofika katika shamba la mifugo la Maloloi lililoko Kijiji cha Milama, Kata ya Dakawa, Wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro, kujionea mfugaji huyo kutoka jamii ya kimasai alivyobadilisha ufugaji wa asili na kuhamia katika ufugaji wa kisasa.

Alisema ni muhimu wafugaji wakabadilika na kuondokana na migogoro ya ardhi kwa kuwa shida za mabadiliko ya hali ya hewa ni endelevu, hivyo ni muhimu kuacha ufugaji wa kuhamahama badala yake wanunue ardhi na kuimiliki kisheria na kufuga mifugo ambayo wana uwezo wa kuipa huduma.

"Ni muhimu wanunue ardhi na waimiliki kwa mujibu wa sheria, inasajiliwa kwa ajili ya ufugaji, anaweka na miundombinu kama majosho na kisima kikubwa cha maji kwa ajili ya uhakika wa kupata maji muda wote, itasaidia sana kufanya sekta hii kuwa na mchango mkubwa," alisema Ulega.

Aliwataka wataalamu wa sekta ya mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) kufika Shamba la Mifugo la Maloloi kumsaidia mmiliki wa shamba hilo kulisajili na kulitambua kuwa ranchi ya sekta binafsi kwa wafugaji wa asili waliobadilika.

Alisema serikali imefanya jitihada za kufungua milango ya biashara kwenye tasnia ya nyama nchi mbalimbali zikiwamo za Saudi Arabia na Oman zinazohitaji nyama kutoka Tanzania, hivyo ni muhimu nchi kuwa na wafugaji wanaofuga kisasa na kuwapo uhakika wa upatikanaji wa nyama bora.

Ulega alisema serikali kupitia Wakala ya Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA), katika kipindi cha miaka mitano, itakuwa ikitoa elimu kwa wafugaji namna bora ya kufuga kisasa, ili wafugaji wengi waanze kufuga kisasa na Tanzania kuendelea kuuza nyama nje ya nchi.

Mmiliki wa Shamba la Mifugo la Maloloi, Maloloi Kibangashi, alisema aliamua kubadilika kwa kuacha kufuga mifugo kwa njia ya asili na kuamua kuuza mifugo hiyo na kununua ng'ombe wa kisasa wa nyama na maziwa ili kuacha ufugaji wa kuhamahama.

Aliwashauri wafugaji wengine kubadilika na kuanza kufuga kisasa kwa kuwa ufugaji wa kuhamahama umekuwa ukisababisha migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima.

Ofisa Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, Natujwa Melau, alisema wilaya hiyo ni miongoni mwa wilaya zenye wafugaji wengi ambao wamekuwa wakihamasishwa kuhusu ufugaji wa kisasa kwa kuwa wengi wao wamekuwa wakiingia kwenye migogoro kwa kupitisha mifugo kwenye mashamba ya wakulima.

Alisema ni muhimu kwa wafugaji kununua maeneo na kuacha ufugaji wa kuhamahama na hivyo kusaidia kuondoa migogoro ya ardhi.



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya bweni ya wasichana ya Nyankumbu wakiwasikiliza viongozi na wafanyakazi wanawake wa Kampuni ya GGML ambao waliwapatia mafunzo ya siku mbili kuhusiana na malezi ya kitaaluma kwa wanafunzi hao wa kike mkoani Geita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ATCL kuongeza ndege mpya tano

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

KAMPUNI ya Ndege (ATCL) imepanga kununua ndege zingine tano ifikapo mwaka 2024 ili kuhimili kasi ya ushindani katika kupanua huduma zake za ndani na nje ya nchi.

Akizungumza katika kikao cha tatu cha Baraza la Wafanyakazi kilichofanyika mjini Morogoro juzi, Mtendaji Mkuu wa ATCL, Ladislaus Matindi, alisema ongezeko hilo litaifanya kampuni hiyo kuwa na jumla ya ndege 17 zitakazosaidia kuchangia maendeleo ya taifa.

Mtendaji huyo Mkuu wa ATCL alisema kuwa mbali na ununuzi huo wa ndege zingine mpya, pia wanatarajia kuongeza safari zao za ndani na nje ya nchi kutokana na kupanuka na kuongezeka kwa shughuli zao.

"Tumepanga kuleta ushindani katika kutoa huduma. Mikakati yetu ni pamoja na kununua ndege zingine tano na kuongeza bidii ya kazi, kuboresha usimamizi pamoja na kukidhi viwango vya ubora unaotarajiwa na wadau wetu mbalimbali wa kitaifa na kimataifa," alisema.

Akifungua kikao hicho, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Mwasa, alisema serikali itaendelea kuwekeza nguvu katika kampuni hiyo ili itoe huduma bora na kuleta ushindani mkubwa.

Alisema tayari ATCL imeanza kufanya vizuri katika kutoa huduma zake kwa kuwa mwaka 2015 kampuni hiyo ilikuwa na ndege moja lakini imeendelea kuongeza ndege hadi kufikia 12 mwaka huu.

Alisema selikali imejipanga kufanya ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege ili kuongeza fursa za kuongezeka kwa safari za ndege na kuruhusu ndege kubwa zaidi kutumia baadhi ya viwanja na huduma zingine zilizo za lazima kwa usafiri wa anga.

Alipongeza kupanuka kwa wigo wa safari za ATCL hadi kuifikia miji ya Lagos (Nigeria), Heathrow (Uingereza), Dubai (Umoja wa Falme za Kiarabu) kwa kuwa kumeleta mafanikio makubwa kwa kampuni hiyo.

Aliwataka ATCL kuhakikisha wanajadili shida zitakazojitokeza kwa namna pana zaidi na wasionekane kama washindani bali watenda kazi na kuweka mikakati mizuri katika kufanikisha utatu-

# Wafanyakazi wanawake GGML wawafunda wanafunzi wa kike

**Na Mwandishi Wetu** GEITA

KATIKA kuhakikisha jamii inanufaika kutokana na shughuli za uchimbaji dhahabu nchini, wafanyakazi wanawake wa Kampuni ya Geita Gold Mine Limited (GGML) wameendesha semina ya siku mbili kwa ajili ya kutoa malezi ya kitaaluma kwa wanafunzi wa kike mkoani Geita.

Semina hiyo iliyofanyika mwishoni mwa wiki mjini Geita katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Nyankumbu iliyojengwa na GGML, ikiasisiwa na kampuni hiyo kupitia Umoja wa Watumishi Wanawake wanaofanya kazi mgodini unaojulikana kwa jina la GGM Ladies.

Akizungumza kwa niaba ya Menejimenti ya GGML, Meneja Mwandamizi - Mawasiliano na Uhusiano, Manace Ndoroma, alisema wanawake wanaofanya kazi mgodini, wamekuwa mstari wa mbele kuhamasisha umuhimu wa nafasi ya mwanamke katika jamii.

Pia alitoa hamasa kwa wanawake kuchangamkia fursa zinazotokana na uchimbaji madini au biashara inayotokana na mnyororo wa thamani katika sekta ya uchimbaji.

Alisema GGML kupitia umoja huo imekuwa ikitoa misaada ya hali na mali ikiwamo fedha na vifaa kwa makundi maalum ndani ya jamii ili kuhakikisha jamii inayozungukwa na shughuli za uchimbaji wa dhahabu, inafaidika kutokana na kuwapo kampuni hiyo.

"Tumekuwa mstari wa mbele kushirikiana na serikali kuhamasisha masuala ya usawa wa kijinsia. Mtakumbuka Agosti 26, mwaka huu, ilikuwa siku maalum ya masuala ya usawa wa kijinsia duniani.

"GGML tulitoa elimu kubwa kwenye mitandao yetu ya kijamii na vyombo vya habari juu ya nafasi muhimu ya mwanamke katika jamii.

"Tumekuwa tukifanya hivyo pia hata katika matukio ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani kila tarehe 8 Machi," alisema Ndoroma na kuongeza kuwa semina hiyo ni mwarobaini wa kero zinazowakabili wanafunzi wa kike kufahamu taaluma sahihi za kuchagua katika maisha baada ya kuhitimu elimu ya sekondari.

Alisema kumekuwapo shida ya wasichana wengi hususani katika mwaka wao wa mwisho wa masomo au baada ya kumaliza elimu ya sekondari, kushindwa kufahamu hatima ya masomo wanayoyasomea na uhalisia wa watakachokutana nacho katika elimu ya juu au baadaye kwenye soko la ajira.

"Sisi Menejimenti ya GGML tuliona ni vyema tuandae semina hii ili hata watakaopenda kuchagua nyanja mbalimbali za taaluma na hata kuwa wachimbaji au viongozi waandamizi katika kampuni za uchimbaji dhahabu, ikiwamo GGML, wafikie ndoto zao kwa kuwaona kinamama wanaofanya vizuri katika taaluma hiyo tuliokuja nao kutoka GGML," alisema Ndoroma.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Geita, Prof. Godius Kahyarara, aliwataka wadau mbalimbali nchini kuchangia maendeleo ya elimu nchini hususani kwa mtoto wa kike badala ya kuiachia serikali jukumu hilo pekee yake.

"Ninawapongeza sana GGM kwa kuonyesha mfano mzuri wa wadau wanaochangia maendeleo ya elimu. Bahati nzuri nchi yetu imeendelea kuwa na mfumo mzuri wa elimu bora ukilinganisha na nchi zingine. GGM wanao mchango mkubwa katika uchumi wa nchi yetu kutokana na kodi wanayolipa.

"Jitihada kubwa wanayoionyesha katika jamii imeleta matokeo chanya ikiwamo kujenga miundombinu ya elimu na mafunzo kama haya yanayoleta tija kubwa katika jamii. Bahati nzuri mafunzo haya yanatolewa kwa wasichana wenye umri mdogo, jambo ambalo siyo rahisi kulisahau," alisema Prof. Kahyarara.

Akihamasisha wanafunzi kufikia ndoto zao katika Shule ya Wasichana Nyankumbu, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Geita, Zahara Michuzi, alipongeza GGML na wafanyakazi wanawake wanaofanya kazi katika kampuni hiyo kwa kuandaa mafunzo hayo yanayotoa mwangaza kwa wanafunzi wengi wa kike kujitambua na kufikia malengo sawa na viongozi wa kike waliofanikiwa katika nafasi mbalimbali.

GGML imekuwa kinara wa uwekezaji kwenye jamii tangu kuanzishwa kwake mwaka 2000 ambapo vipaumbele vikuu vimekuwa ni miradi ya afya, elimu, maji, barabara, miradi ya kukuza kipato na miradi mingine mingi ya kijamii ili kuhakikisha jamii mwenyeji inapata maisha bora.

Kampuni hiyo imejenga shule saba za msingi na tano za sekondari ndani ya Mkoa wa Geita kwa kipindi cha miaka minne iliyopita.

Mapema mwaka huu, GGML ilibuka mshindi wa jumla katika kampuni zinazofanya vizuri kwenye sekta ya madini nchini kwa mwaka 2020/21 baada ya kunyakua tuzo katika vipengele vya uwajibikaji wa kampuni kwa jamii, mazingira, usalama, mlipaji bora wa kodi na uendelezaji wazawa.

HABARI KITAIFA

# Wajawazito watoa kilio cha ubovu wa barabara

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAJAWAZITO katika kijiji cha Mwashagi Kata ya Lyabukande Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, mkoani Shinyanga, wanalazimika kujifungulia kwenye majaruba ya mpunga wakati wakipelekwa hospitali kutokana na ukosefu wa zahanati na ubovu wa barabara.

Wamesema wanakumbwa na tatizo hilo kipindi cha msimu wa mvua kutokana na barabara kutopitika wanapokwenda kufuata huduma ya afya makao makuu ya kata, umbali wa zaidi ya kilomita tano na kusababisha wajawazito kuanguka kwenye majaruba ya mpunga na wengine kujifungulia humo.

Wananchi wa kijiji hicho walipaza sauti zao mwishoni mwa wiki wakati Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, alipofanya ziara kijijini humo ya kukagua utekelezaji wa mradi wa majisafi na salama ambao umekamilika kwa asilimia 98 na kuanza kutoa maji.

Mmoja wa wananchi hao Maguta Jilili, alipongeza serikali kwa kuwapelekea huduma ya majisafi na salama.

Alisema licha ya kupata huduma hiyo, bado wanakabiliwa na tatizo la ubovu wa miundombinu ya barabara.

"Mvua zikinyesha barabara kwenye kijiji hiki hazipitiki na hata wewe Mkuu wa wilaya umejionea mwenyewe, inatulazimu kupita juu ya kingo za majaruba, tabu inakuja kwa wajawazito namna ya kupita na wengine huanguka na kujifungua humo humo," alisema Jilili.

Mbaru Minza, kwa upande wake alisema wanapata shida kupata huduma ya kujifungua na kuiomba serikali kukarabati miundombinu ya barabara pamoja na kuwajengea zahanati.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, alisema tayari alishaagiza Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kukarabati miundombinu ya barabara kijijini humo, huku akiwapongeza wananchi kwa kujitoa kuchangia shughuli za maendeleo, ikiwamo kuanza kujenga zahanati kwa nguvu zao.



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, akionyesha kitabu cha miongozo ya usimamizi na uendeshaji wa elimu ngazi ya mkoa baada ya uzinduzi wake katika hafla iliyofanyika kwenye ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Songea Girls mwishoni mwa wiki. **PICHA: GIDEON MWAKANOSYA**

# Serikali yazionya shule zinazochuja wanafunzi

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imepiga marufuku baadhi ya shule kuchuja wanafunzi wasiofikia kiwango na kuwazuia kufanya mitihani ya kitaifa ambao hawajakamilisha ada zao.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhaji Abdul Maulid, alipiga marufuku hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali ya 19 ya shule ya St Anne Marie Academy, Mbezi Kimara.

Alisema serikali haikubaliani na hali hiyo ambayo huwasababishia wazazi msongo wa mawazo wanapopewa taarifa za watoto kuchujwa kwa kushindwa kufikia viwango.

"Unakuta mtoto amesoma hapo darasa la kwanza mpaka la saba au kidato cha kwanza mpaka cha nne, wakati wa mtihani shule inaweka vigezo vyake kwamba huyu aondoke, aondoke aende wapi wakati muda wote amesoma shuleni kwako. Hiyo hatutakubali tunataka amalizie hapohapo kwako alikoanzia na hatutaki arudie darasa," alionya.

"Mtoto amekuja kwako akiwa vizuri umekaa naye na kama kuharibika kaharibikia shuleni kwako sasa unataka kumpeleka kwa nani? Hii haikubaliki hata kidogo tupeni taarifa ya shule hizo zenye tabia ya kuondoa watoto kwenye siku za mitihani," alisisitiza.

Maulid alisema lipo tatizo lingine la wanafunzi kukataliwa kufanya mitihani yao ya mwisho kutokana na kushindwa kumaliza ada jambo ambalo alisema serikali haitalivumilia.

"Mtoto amekuja kusoma mkataba ni kati ya shule na mzazi, lakini anapofika darasa la saba au kidato cha nne anarudishwa nyumbani eti hajalipa ada, hakuna sheria inayoruhusu mtoto kurudia darasa kwasababu hajalipa ada, mtoto anarudia darasa iwapo anaumwa hivyo shule za Dar es Salaam zungumzeni na wazazi kabla ya mtihani mmalizane msisumbue watoto." Maulid alisema amefurahishwa na ubora wa elimu unaotolewa na shule hiyo ambayo imekuwa ikiongoza Mkoa wa Dar es Salaam na Wilaya ya Ubungo na kuingia kwenye kumi bora kitaifa mara kwa mara.

"Kuna usemi kwamba usione vyaelea vimeumbwa maana umahiri wa wanafunzi niliouona hapa leo ni jitihada za walimu na menejimenti ya shule nawapongeza sana, shule ziko nyingi sana ila nimeamua kuja hapa St Anne Marie kwasababu hakuna longo longo hapa," alisema.

"Mimi ni Ofisa Elimu wa Mkoa, Mkuu wangu wa mkoa anajua leo St Anne Marie kuna nini na ameniambia nije hapa na pia kuna Mkurugenzi wa Halmashauri kuna Ofisa Elimu wa wilaya hapa, mheshimiwa diwani naye yupo hapa, wazazi mmechagua shule bora na hamjakosea kuwaleta watoto wenu hapa," alisema.

Aliwataka wazazi kuwalinda watoto dhidi ya ukatili na wasimwamini mtu kuhusu ulinzi wa watoto wao kutokana na vitendo vya ukatili dhidi yao kuongezeka.

"Watoto hawa ndiyo tunawategemea wapatikane kina Rweikiza, kina Maulid, mama Samia, hivyo tusiwachezee watoto hawa, mwanajamii ukiona mtoto anafanyiwa ukatili toa taarifa, shule zifanye kama St Anne Marie ziajiri wasimamizi wenye weledi wa hali ya juu," alisema.

# Tanzania ya tatu Afrika uzalishaji mazao mikunde

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

TANZANIA imeshika nafasi ya tatu katika nchi za Afrika kwa uzalishaji wa mazao ya mikunde baada ya kuuza nje ya nchi tani 455,304 katika kipindi cha msimu wa mwaka 2021 na kuliingizia taifa fedha za kigeni inayoongoza ni Nigeria na pili ni Niger.

Mbaazi imechangia asilimia 46 kiwango ambacho ni kikubwa ikilinganishwa na mazao mengine ya jamii hiyo.

Mtafiti Mwandamizi wa mazao ya mikunde nchini kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Ilonga iliyoko wilayani Kilosa, mkoani Morogoro, Meshack Makenge, alisema hayo wakati wa kikao kazi kilichofanyika mkoani humo na kushirikisha wadau wa mazao hayo.

Kikao kazi hicho kilikuwa kinafanya tathmini ya kuweka mikakati katika mradi wa uendeshaji na upatikanaji wa mbegu bora za mazao jamii ya mikunde na nafaka Afrika (AVISA) ambao unasimamiwa na TARI Ilonga.

Makenge alisema licha ya Tanzania kuuza nje mazao ya mikunde, bado mahitaji ni makubwa ya mazao hayo nje ya nchi inayofikia wastani wa tani milioni moja kwa mwaka na kupitia mradi wa AVISA wameweka mikakati ya kuongeza uzalishaji wa mbegu bora.

"Hivi sasa soko la mazao ya mikunde limefunguka hapa nchini kuna viwanda vya kutosha kimoja kipo hapa Morogoro, lakini wenzetu wa India wanahitaji sana hivyo kupitia mradi wa AVISA tumelenga kuzalishaji mbegu za kisasa na kuwapatia wakulima wazalishe," alisema Makenge.

Mratibu wa Mradi wa AVISA, Emmanuel Mwenda, alisema mradi huo ulianza kutekelezwa mwaka 2019 katika nchi saba Tanzania ikiwa mojawapo na umelenga mazao ya maharagwe, mbaazi, dengu, ulezi, mtama na karanga.

Alisema mazao ya dengu na mbaazi yameongezwa katika mradi huo katika kipindi cha mwaka 2021/22 kutokana na kufanya vizuri katika soko, lakini tija yake ni ndogo kutokana na uzalishaji kwa wakulima kuwa chini.

Alisema kwa hapa nchini mazao ya mbaazi na dengu yamekuwa yakilimwa kwa muda mrefu, lakini wakulima wanatumia mbegu za asili na kutotumia kanuni bora za kilimo na kusababisha tija yake kuwa ndogo na mradi huo utazalisha mbegu za teknolojia ya kisasa ili waweze kuongeza tija.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa TARI Ilonga, Dk. Emmanuel Chilagane, alisema mazao jamii ya mikunde yana faida nyingi zikiwamo lishe ya binadamu hususani protini, malisho ya mifugo, malighafi ya viwanda, kuboresha afya ya udongo na kutunza mazingira.

Akifungua kikao kazi hicho, Mkurugenzi wa Utafiti na Ubunifu kutoka TARI makao makuu, Dk. Joseph Ndunguru, alisema mradi huo unaunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan katika agenda yake ya 10/30 ya kukuza kilimo na kukifanya kuwa cha kibiashara kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

Alisema kupitia mradi huo, wakulima watapata mbegu za teknolojia ya kisasa na elimu ya kilimo bora ili kuongeza uzalishaji wenye tija kwa kuwa tayari serikali imeshasaini makubaliano ya kuuza mazao ya mikunde katika nchi ya India.

# Wanafunzi 42 vyuo vikuu wahitimu mafunzo ya ubunifu

**Na Renatha Msungu**

TUME ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), imefunga programu yake ya kuibua vijana wenye vipaji kutoka vyuo vikuu, inayofahamika 'Buni Talent Hub' kwa mwaka 2022 iliyojumuisha wanafunzi 42 kutoka vyuo vya elimu ya juu nchini.

Wahitimu hao wamebuni bunifu mbalimbali na kuziwasilisha kwa jamii ili kuona kama zinatija kwa ajili ya kubadilisha kuwa bidhaa za huduma.

Akizungumza wakati wa kufunga mafunzo hayo, mwishoni mwa wiki, jijini Dar es Salaam, Mtaalamu wa Mahusiano wa Kumbi ya Ubunifu ya Buni Hub, Promise Mwakale, alisema programu hiyo ilianza Julai mwaka huu hadi Septemba na ilichukua wanafunzi 42 kutoka vyuo vikuu vinne.

Mwakale alivitaja vyuo vilivyotoa washiriki kuwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Taasisi ya Uhasibu (TIA) na Chuo cha Ardhi.

Mwakale alisema kupitia programu hiyo, vijana hao wamefanikiwa kuandaa bunifu mbalimbali ambazo waliziwasilisha kwa jamii ili kuona kama zinatija kwa ajili ya kuzibadilisha kuwa bidhaa au huduma.

"Tunamaliza programu ya Talent Hub ambayo vijana 42 wanahitimu, wanamaliza mafunzo ya wiki kumi yaliyoanza toka Julai hapa COSTESH na wamepitia kuangalia mawazo yao, kutengeneza timu, wakabadilishana mawazo kwa ajili ya kuyaweka vizuri," alisema Mwakale.

Alisema programu hiyo kwa sasa ina mwaka wa saba na imesaidia vijana wengi kujiajiri na kujikwamua kiuchumi.

Kwa upande wake mhitimu wa programu hiyo, Ibrahim Laseko, alisema imewapa nafasi ya kujifunza kuandaa wazo kutokana na changamoto zinazoikabili jamii, kikundi chake kimeanzisha mtandao unaofahamika jina la Kazi Faster, ambao huwakutanisha waajiri na watu wanaotafuta kazi.

"Tulipanga wazo na kwa sasa application tunayoifanyia kazi inaitwa Kazi Faster, ila haijakamilika na itakuwa App ndani ya muda mchache na tumelenga watumiaji watakuwa vijana ambao wenye uwezo wa kuingia kwenye mtandao kufanya kazi mbalimbali ili kujipatia kipato," alisema Laseko.

Alisema hiyo itasaidia kuondokana na watu kukaa vijiweni na kusikilizia kazi ambazo hazipo badala yake watakuwa bize na kazi za mitandao.

Naye Teddy Micky kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi, alisema "Programu ya Buni wanapata nafasi ya kujua jinsi gani wanaweza kuendeleza au kuanzisha biashara au kuandaa kitu kipya kwa ajili ya jamii yao.

Alisema wamejifunza jinsi gani wanaweza kufanya biashara au kitu wanachotaka kuanzisha kwenye sayansi na teknolojia.

Teddy alisema, katika kundi lake lililotoka na programu hiyo, wamefanikiwa kuanzisha mtandao 'Application' inayopatikana katika simu za kiganjani, kwa ajili ya kuwakutanisha wagonjwa na madaktari.

"Mimi na kundi langu tumeweza kuanzisha App ambayo itasaidia mgonjwa kumuita daktari nyumbani na kupata huduma hapo alipo. Lakini pia tumepata kujua vitu mbalimbali katika jamii hasa kwa kuangalia maisha halisi ya Watanzania na kutatua changamoto za kila siku katika jamii yetu," alisema Teddy.

# DC awaonya wanaojaribu kuhujumu mradi Tembo Nickel

**Na Mwandishi Wetu,**
NGARA

MKUU wa Wilaya ya Ngara, Kanali Mathias Kahabi, amesema mtu atakayejaribu kuhujumu mradi wa uchimbaji madini wa Tembo Nickel, atakuwa anaihujumu serikali na hatokubali itokee.

Kanali Kahabi aliyasema hayo alipokuwa akizungumza kwa nyakati tofauti katika vijiji vya Rwinyana na Bugarama, alipofanya ziara ya kuzungumza na wananchi umuhimu wa uthaminishaji mali na makazi kwa wananchi wanaozunguka eneo la mradi wa Tembo Nickel wilayani Ngara.

"Mradi huu ni mkubwa, tusiuchukulie poa, ni mradi wa kimkakati, kampuni kubwa kutoka nje ya Tanzania imewekeza pale, Tanzania tuna asilimia 16 kwenye huo mradi, mwekezaji ana asilimia 84 ni uwekezaji mkubwa utakao tufaidisha.

"Kwa maana hiyo sisi ndiyo walinzi namba moja wa huu mradi, mimi kama mlinzi wa usalama ni jukumu langu kuhakikisha unafanikiwa na hakuna mtu wa kuuchezea, ukijaribu kuhujumu huu mradi ujue unaihujumu serikali na mimi sintokubali hilo litokee na serikali ya mkoa haitokubali," alisema.

Pia alisema kuna watu wametoka maeneo mbalimbali ikiwamo Geita na Mwanza ili kurubuni wananchi wa vijiji vinavyozunguka mradi huo wawauzie maeneo yao baada ya tarehe ya katazo la kuendeleza makazi na mashamba kutolewa.

"Wamekuja wakanunua mashamba kwa hela ndogo, tegesha ni matapeli wanataka kuvuruga zoezi zima la uthamini, lakini wajue hizi kazi za miradi mikubwa zinafanyika kitaalamu mno, kuna picha za satelaiti zilishachukuliwa tangu Julai 18, mwaka huu, kila kilichoko shambani kinajulikana.

"Rai yangu kwenu naomba mtoe ushirikiano kwa wathamini, wanafanya shughuli zao kitaalamu sana ili kuhakikisha kila mtu anapimiwa na kuhesabiwa mali zake na alipwe kile anachostahili," alisema.

Alisema macho na masikio ya serikali kwa sasa yapo kwenye mradi huo wa Tembo Nickel na kuwaonya viongozi wa vijiji wanaokubali kurubuniwa na wanaotaka kununua ardhi na kuendeleza maeneo yao.

"Tuna taarifa kwa viongozi wa vijiji kuingiza watu wahuni kwenye kamati nyeti za ardhi, tegesha wanawakatia maeneo humo, Rusumo walingiza wahuni wakaathiri zoezi huko, huku hatutokubali hilo lijitokeze.

"Tunajua pia kuna wanaume walikuwa wameacha wake na watoto wakakimbia huko kwenye eneo la mradi, sasa wanarudi huko wanauza nyumba na mashamba bila kujali watoto wataenda wapi, yote hayo hatutakubali kwasababu tunajua yatatuletea shida huko mbele," alisema.

Mshauri Elekezi wa Mpango wa uhamishaji watu na makazi katika mradi wa Tembo Nickel, kutoka kampuni ya RSK, Basil Shio, alisema wanaendesha kazi ya uthamini kwa kufuata sheria na taratibu za nchi na sasa hivi wamefikia asilimia 40 katika vijiji vinavyoguswa na mradi huo.

"Kuna maeneo hatujamaliza na kikubwa ni kwasababu ya migogoro ya mipaka, mthamini hawezi kufanya kazi maeneo yenye migogoro.

Kwa sasa tupo kwenye Kijiji cha Rwinyana, tulijipangia miezi minne ya kuchukua taarifa uwandani, sasa hivi tunamalizia mwezi wa pili wathamini wakiwa uwandani na hadi sasa tupo kwenye asilimia 40, tumeshafikia wananchi zaidi ya 549 na kupima vipande vya ardhi zaidi ya 900," alisema.




Mshauri Elekezi wa Mpango wa Uhamishaji Watu na Makazi katika mradi wa Tembo Nickel kutoka Kampuni ya RSK, Basil Shio (kulia), akimwonyesha Mkuu wa Wilaya ya Ngara, Kanali Mathias Kahabi (katikati), maeneo ambayo yameshafanyiwa uthamini ili kupisha mgodi wa uchimbaji madini ya Nickel, (aliyevaa miwani) ni Kiongozi wa Kitengo cha Mahusiano kwa Jamii kutoka kampuni hiyo, Francis Wikedzi.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima korosho wapewa viuatilifu kudhibiti wadudu

**Na Ibrahim Yassin, SONGWE**

KATIKA kuhakikisha wakulima wa zao la korosho wilayani Songwe wanaendelea kujikita kwenye kilimo hicho, wilaya imetoa viuatilifu vya kupambana na wadudu waharibifu mashambani.

Makabidhiano ya viuatilifu hivyo yamefanywa na Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Simon Simalenga, akisaidiana na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe, Ofisa Kilimo na baadhi ya wakulima.

Simalenga, aliwapongeza wakulima kwa kuitikia wito wa serikali wa kuanza kulima zao hilo, akisema korosho ni zao la kimkakati wilayani humo litakalokuza kipato cha wananchi na kuwatoa katika lindi la umaskini.

"Niwapongeze sana wakulima kwa kuitikia wito wa serikali, mkulima kwa kufuata ushauri wa wataalamu mtainuka kiuchumi," alisema Simalenga.

Pia, ameitaka Idara ya Kilimo kuweka utaratibu wa kuwatembelea wakulima wa mazao mengine ili kutatua kero na kuwapa elimu kuhusu zao husika ili waweze kuhamasika zaidi.

Makamu Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Wangala Wangala, akizungumza kwa niaba ya Mwenyekiti wa Halmashauri, Abraham Sambila, alisema wameafikiana kama Baraza la Madiwani kuwa na utaratibu wa kwenda kujionea mashamba ya wakulima na kuwahamasisha, zoezi hilo litaanza mwezi Oktoba.

Andrew Kayombo, Ofisa Kilimo wilayani Songwe alisema awali kulikuwa na dhana potofu kuwa korosho haiwezi kulimwa wilayani humo, lakini kupitia ushuhuda wa baadhi ya wakulima wamehamasika na eneo lolote ambalo mwembe unaweza kuota na kukua pia korosho inawezekana.

Baadhi ya wakulima wa zao hilo akiwamo Radislaus Selemani mwenye hekari 15 na Charles Shalumbuzi wameishukuru serikali kwa kuwapatia viuatilifu kwa muda mwafaka ili kudhibiti magonjwa kama 'ubwili wa unga' ambao huwa tatizo kubwa kipindi cha kiangazi kwa zao la korosho.

Dawa zilizotolewa ni Subachlo (udhibiti wadudu), Movil (kudhibiti magonjwa ya fangasi kama ubwili unga), na Indazole, huku wakulima wakionesha tabasamu tayari kwa kuanza kulima zao hilo.

Nipashe Spotika




WACHEZAJI 5 WENYE KIWANGO BORA ZAIDI KWA SASA DUNIANI UK. 12-13

# SABABU 3 HUU UNAWEZA KUWA MSIMU MBAYA KWA RONALDO




**MANCHESTER,** England

DIRISHA la usajili la majira ya joto lilifungwa Septemba Mosi, mwaka huu na harakati za mshambuliaji wa Manchester United, Cristiano Ronaldo kutaka kuondoka ziligonga mwamba.

Hapo awali alikuwa ameiarifu klabu kuhusu nia yake ya kuondoka pale Old Trafford ili kwenda kujiunga na klabu inayocheza Ligi ya Mabingwa Ulaya. Hata hivyo, kusita kwa United pamoja na kutovutiwa na klabu nyingine katika kumsajili kumemfanya ashushwe kwenye benchi la 'Mashetani Wekundu' hao.

Akitajwa kuwa mmoja wa wanasoka bora wa wakati wote, mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or amefikia hatua za mwisho za maisha yake ya soka. Hilo ndilo lililomsukuma kutaka kuhamia klabu inayocheza Ligi ya Mabingwa Ulaya. Hata hivyo, klabu kubwa kama Bayern Munich, Atletico Madrid na Chelsea, licha ya kuhusishwa naye, zilikana mpango wa kumsajili nahodha huyo wa Ureno.

Na sasa Ronaldo amebaki Old Trafford msimu huu. Hata hivyo, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37, akiwa tayari ameshuka kwenye benchi, muda wake United unaweza kuwa katika kipindi kigumu sana msimu huu.

Hizi ni sababu tatu kwa nini Ronaldo anaweza kuwa na msimu wake mbaya zaidi uwahi kutokea katika maisha yake yka soka msimu huu...

**#3. Hafai mtindo mpya wa uchezaji wa Man United**

Wakati United ilipomtimua Ole Gunnar Solskjaer na kumleta Ralf Rangnick, Mjerumani huyo alitekeleza uchezaji wa kushambulia kwa kasi. Changamoto yake kubwa katika hatua hiyo ya ushambuliaji ilikuwa kumfanya mkongwe huyo aende mbio akiwania mpira katika nafasi ya tatu ya mwisho.

Ronaldo alishindwa kuleta nguvu hizo kutokana na umri wake. Hata hivyo, tatizo lilizidi kuwa gumu ingawa aliendelea kufunga mara kwa mara licha ya kutoendana na aina ya uchezaji wa timu hiyo. Ilisababisha Ronaldo kuhusika na kuwajibika kwa soka zuri na baya liliyochezwa na klabu.

Ronaldo uchezaji wake wa polepole mbele ulizuia uwezo wa timu kucheza kwa kasi kama kocha alivyokuwa anataka.

Kuwasili kwa Erik ten Hag kulitoa mwelekeo kwa tatizo hilo. Bosi huyo wa Uholanzi aliendelea na mtindo huo wa soka la kasi kwa kila mtu, akiwamo Ronaldo. Ingawa aliboresha uchezaji wa timu ya United, Ronaldo haonekani tena kuwa mchezaji sawa na alivyokuwa msimu uliopita.

Ameanza mechi moja tu za ligi msimu huu, dhidi ya Brentford. United wakipoteza kwa mabao 4-0 katika mchezo huo. Kauli kubwa ilikuja wakati Ronaldo alipowekwa benchi katika ushindi wa mabao 2-1 wa United dhidi ya Liverpool.

Msimu huu unaweza kuwa mbaya zaidi kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37. United wanacheza sana na washambuliaji wao wadogo na Ronaldo asipobadilisha mchezo wake, kuna uwezekano mkubwa wa kukosa kabisa nafasi ya kucheza kwa 'Mashetani Wekundu' hao.

**#2. Kukosa Ligi ya Mabingwa Ulaya**

Ronaldo amekosa kushiriki michuano hiyo kwa mara ya kwanza tangu ajiunge na Manchester United mwaka wa 2003. Badala yake atakuwa kwenye hesabu ya mechi za Alhamisi usiku kwenye Ligi ya Europa.

Tatizo hapa ni kwamba Ronaldo ni mtu mwenye ari kubwa. Anafurahia mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, kitu ambacho huleta ubora zaidi ndani yake. Kukosa kucheza dhidi ya wachezaji bora kunaweza kusababisha kushuka kwa kasi ya Ronaldo kuliko ilivyotarajiwa.

**#1. Amepoteza sapoti ya wachezaji wenzake**

Ujio wa Ronaldo pale Old Trafford msimu uliopita wa majira ya joto ulipokelewa kwa shangwe na nderemo kwenye kambi ya Manchester United. Hata hivyo, katika kipindi cha msimu huu, inasemekana amekuwa akizozana na wachezaji kadhaa kuhusu mtazamo na kujitolea kwao.

Halafu kulikuwa na mahitaji yake yote ya kutaka kuhama msimu huu wa majira ya joto kwani hakuamini kuwa wachezaji wenzake walikuwa wazuri vya kutosha. Kubaki kwa Ronaldo klabuni hapo inaeleweka kwamba wachezaji wenzake hawatamkubali kwa ukarimu.

Baada ya kuchapwa mabao 4-0 na Brentford, msaidizi wa Ten Hag, Steve McClaren, alionekana akimtaka Ronaldo kuwapongeza mashabiki wa ugenini. Ronaldo alichagua kumpuuza na akaondoka.

Muungano kati ya Ronaldo na Manchester United unaonekana kuwa haufai kwa sasa na huu unaweza kuwa msimu mrefu zaidi kwake.

## ISIKUPITE

KWENYE Ligi Kuu England, Cesc Fabregas ndiye mchezaji anayeshikilia rekodi ya mchezaji mwenye pasi nyingi za mwisho 'assists' (38) kabla ya kufikisha umri wa miaka 21, akifuatiwa na Wayne Rooney (22), Michael Owen (18) na Bukayo Saka (18).



# WACHEZAJI 5 WENYE KIWANGO BORA ZAIDI KWA SASA DUNIANI



HAALAND

**LONDON,** England

MSIMU wa 2022-23 ulianza kote Ulaya Agosti mwaka huu. Na dirisha lingine la kufurahisha la uhamisho wa majira ya joto lilifungwa Septemba Mosi na tunajua kwa hakika kwamba huu utakuwa ni msimu bora zaidi kwa soka duniani.

**Baadhi ya timu kuna wachezaji tayari wameweka alama kwa ajili ya changamoto katika nyanja zote za msimu huu. Mfumo wa msimu wa mapema ni muhimu sana kwani huweka sauti kwa kampeni iliyosalia na huboresha hali ya kujiamini ya mchezaji mara mambo yanapoanza kuwa makali zaidi.**

Bila kuchelewa zaidi, hebu tuangalie wachezaji watano walio katika kiwango bora zaidi duniani kwa sasa.

**#5. Aleksandar Mitrovic (Fulham)**

Aleksandar Mitrovic amekuwa na mwanzo wa kushangaza kwa mwezi wake wa kwanza wa msimu mpya wa Ligi Kuu ya England. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Serbia pia alikuwa katika kiwango kizuri cha ufungaji katika mwaka uliopita pia. Amefunga mabao 49 katika mechi 49 zilizopita za ligi akiwa na Fulham.

Mitrovic anajiamini kwa sasa na amefunga mabao sita katika mechi sita katika msimu wa Ligi Kuu England. Amesajili mikwaju 27 kwenye Ligi Kuu England hadi sasa msimu huu na hiyo ndiyo mikwaju mingi zaidi ya mchezaji yeyote kwenye ligi.

Hili halionyeshi tu njaa ya Mitrovic bali pia ni straika ambaye ana uwezo wa kuingia kwenye nafasi nzuri mara kwa mara ili kupata mkwaju wake. Kiwango cha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, kimekuwa muhimu kwa Fulham kukaa katika nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England baada ya mechi sita.

**#4. Kylian Mbappe (Paris Saint-Germain)**

Safu nzima ya ushambuliaji ya Paris Saint-Germain imekuwa katika hali nzuri msimu huu mpya. Baada ya kusaini mkataba mpya na klabu hiyo kipindi cha majira ya joto, Kylian Mbappe ameanza kufanya kazi ya kushikilia ubavu wake kwa kuwa katika kiwango cha kuvutia.

Kasi yake ya kusisimua, uelekevu na harakati zake za kiakili humfanya aonekana mtu muhimu sana kwenye safu ya watatu ya kushambulia. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, amefunga mabao saba katika mechi sita za Ligue 1 hadi sasa msimu huu na anaonekana kuwa na kampeni kubwa zaidi.

**#3. Lionel Messi (Paris Saint-Germain)**

Lionel Messi hatimaye ameanza kufurahia maisha pale Paris. Baada ya kampeni mbaya ya kwanza akiwa na Paris Saint-Germain, Messi anatamba kwenye viunga vya Parc des Princes msimu huu. Uamuzi wa kocha mpya, Christophe Galtier kumhamisha Messi kwenye nafasi muhimu zaidi umefanya maajabu kwa mchezaji na timu.

Mshindi huyo mara saba wa Ballon d'Or anatumika kama kiungo mshambuliaji msimu huu. Hii imeisaidia PSG kutumia vema uwezo wa ajabu wa uchezaji wa Messi. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, amekuwa kiungo kati ya safu ya kiungo na ushambuliaji na amefanya kazi nzuri hadi sasa.

Katika mechi sita za Ligue 1 hadi sasa msimu huu, Messi amefunga mabao matatu na kutoa asisti tano.

**#2. Erling Haaland (Manchester City)**

Wakati Erling Haaland akijiunga na Manchester City, kulikuwa na wasiwasi kama angekuwa anafaa kwa kikosi cha Pep Guardiola. Imemchukua Haaland mwezi mmoja kuwanyamazisha wakosoaji wake.

Mshambulizi huyo wa Norway ameingia kwenye ndoto kamili ya kuanza maisha katika Ligi Kuu. Amefunga mabao 10 na kutoa asisti moja katika mechi sita kwenye Ligi Kuu England hadi sasa msimu huu.

Haaland alifunga 'hat-trick (mabao matatu) mfululizo katika mechi yake ya nne na ya tano ya Ligi Kuu dhidi ya Crystal Palace na Nottingham Forest.

Anaonekana kila kukicha mnyama mkubwa ambaye alitikisa kabisa Bundesliga katika misimu michache iliyopita. Hakuna shaka kwamba yeye ndiye kitu kikubwa kinachofuata kwenye soka.

**#1. Neymar Jr. (Paris Saint-Germain)**

Neymar Jr. hakushiriki sana kwa PSG katika msimu wa 2021-22 kutokana na matatizo mengi ya majeraha. Hata alizomewa mara nyingi na mashabiki wa kikosi hicho chenye maskani yake pale Parc des Princes baada ya timu hiyo kuondolewa katika raundi ya 16 ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Lakini mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Brazil amekuwa na mwanzo mzuri sana wa msimu huu. Neymar amekuwa moto kwa PSG msimu wa 2022-23 hadi sasa. Amekuwa akijawa na kujiamini na ameonekana kutisha.

Huku Messi akicheza nyuma yake, Neymar ametumia muda mwingi kwenye safu ya ushambuliaji na huko ndiko kwenye hatari yake zaidi. Mbinu yake ya kupendeza, akili na harakati zimemfanya aonekane kutozuilika hadi sasa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, amefunga mabao saba na kutoa pasi za mabao sita katika mechi sita za Ligue 1 hadi sasa msimu huu.

## Nukuu

"Katika maisha yangu, nimeona wachezaji wachache sana ambao wanatajwa kuwa bora zaidi katika historia. Lionel Messi, kwangu, ndiye bora zaidi kuwahi kuona. Nina mgawanyiko kidogo kati yake na Ronaldo Nazario," **Mshambuliaji wa Arsenal, Gabriel Jesus**




"Nadhani ninakaribia kushinda [Ballon d'Or]. Mimi mara zote nasema nina ndoto ya kila kitu. Sina kizuizi. Kwa hiyo, kama unavyosema, ni kizazi kipya. Na Ronaldo, Messi - watapita. Tunapaswa kutafuta mtu mwingine, mtu mpya. Kila mwaka nilijiuliza nani atashinda Ballon d'Or, Messi au Cristiano. Napendelea nani? Ni sawa na kuchagua kati ya baba yako au mama yako, huwezi," **Mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe**



"Kucheza dhidi ya Virgil van Dijk ni ngumu kwa sababu kama beki wa kati, ana nguvu na akili. Anajua ni wakati gani mwafaka wa kukuasha na wakati wa kuingia kwa ajili ya kukupokonya mpira. Hiyo inafanya kuwa ngumu zaidi. Ni ngumu zaidi kucheza dhidi ya mabeki wa kati wenye akili. Hawafanyi makosa." **Mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Neymar akisifia ubora wa beki wa Liverpool, Van Dijk.**





Straika Fiston Mayele (kushoto), ambaye alipiga 'hat-trick' kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika juzi, akimtoka mmoja wa walinzi wa Zalan FC ya Sudan Kusini katika mechi ya hatua ya awali iliyochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa na Yanga kushinda mabao 4-0 juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# SIMBA, YANGA NA REKODI ZAO MECHI CAF

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA kile kinachoonekana ni nadra sana kutokea kwenye soka la Tanzania, timu mbili kongwe na zenye mashabiki wengi, Simba na Yanga kila moja juzi ilipata ushindi kwenye mechi za kimataifa zilizochezwa siku moja na wakati mmoja.

**Mabingwa wa Tanzania Bara wakiwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, lakini kikanuni wakiwa ugenini, waliichakaza Zalan FC mabao 4-0 kwenye mechi ya raundi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kujiweka mazingira mazuri ya kutinga raundi ya kwanza zitakaporudiana Septemba 17, mwaka huu hapa hapa nchini kwenye uwanja huo huo.**

Wawakilishi wengine wa Tanzania kwenye mechi za kimataifa, Simba walikuwa ugenini nchini Malawi kwenye Uwanja wa Bingu Mutharika, Lilongwe ambako ilifanya mauaji kwa kuisulubu Nyasa Big Bullets mabao 2-0.

Simba nayo inahitaji ushindi, sare au kutofungwa zaidi ya bao 1-0 moja kwenye mechi ya marudiano Septemba 18, Uwanja wa Benjamin Mkapa ili kutinga kwenye raundi ya kwanza ya michuano hiyo barani Afrika.

Makala haya tunaangalia matukio, na rekodi zilizowekwa na timu pamoja na wachezaji kwenye mechi hizo.

**Yanga baada ya miaka sita**

Ushindi wa juzi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika umeifanya timu hiyo kushinda mechi kwa mara ya kwanza baada ya miaka sita.

Mara ya mwisho kupata ushindi kwenye Ligi ya Mabingwa ilikuwa Februari 27, 2016 ilipoifunga Cercle de Joachim ya Mauritius mabao 2-0 ugenini yakifungwa na Amisi Tambwe na Thabaani Kamusoko.

Pia mara ya mwisho Yanga kushinda kwenye Ligi ya Mabingwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa ilikuwa dhidi ya timu hiyo hiyo, Februari 13, ikishinda bao 1-0 kupitia kwa Donald Ngoma.

**Mayele ndani rekodi ya 'hat-trick'**

Straika Mkongomani Fiston Mayele, ameweka rekodi ya kufunga mabao matatu kwenye mechi moja dakika ya 46, 85 na 89 na kuweka rekodi zilizowahi kuwekwa na wachezaji waliocheza ligi ya Tanzania waliowahi kufanya hivyo ambao ni Mrisho Ngassa 2014 kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa, Yanga ikiichapa Comorozine mabao 7-0, kiungo huyo akipiga mabao hat-trick kwenye mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Taifa.

Miaka miwili baadaye mchezaji raia wa Ivory Coast aliyekuwa akicheza kama kiungo mshambuliaji wakati mwingine straika, Kipre Tchetche alipiga hat-trick kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, timu yake ikishinda mabao 4-3 dhidi ya Bidvest Wits ya Afrika Kusini, mechi ikichezwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi mwaka 2016.

**Yanga hatari kipindi cha pili**

Kama ilivyokuwa kwenye Ligi Kuu, Yanga inaonekana kuwa hatari zaidi kipindi cha pili. Kwenye mechi za ligi pamoja na juzi imethibitika hivyo, kwani mabao yote manne yalifungwa kipindi cha pili.

Tumeona kwenye mechi za ligi hata kama timu hiyo haijafunga bao, au ikiwa nyuma, inaingia uwanjani ikiwa imebadilika kabisa na kuweza kubadili matokeo, ikarudisha mabao, au kushinda kabisa.

**Simba ugenini ndiyo zake**

Kwa sasa inaanza kuonekana kuwa Simba kushinda ugenini si jambo la ajabu tena. Ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Nyasa Big Bullets umekuwa ni wa tano kushinda ikicheza ugenini kwa miaka mitano ambayo timu hiyo imefanya makubwa kwenye michuano ya kimataifa.

Desemba 4, 2018 iliichapa Mbabane Swallows ya Eswatini mabao 4-0 ikiwa nchini humo, Novemba 29, 2020 iliidungua Plateau United bao 1-0 nchini Nigeria, Februari 12, 2021 iliibamiza AS Vita Club bao 1-0 nchini DR Congo na Oktoba 27, 2021 iliifunga Jwaneng Galaxy mabao 2-0 nchini Botswana.

**'Tiktak' ya Phiri kama Sakho**

Bao la kwanza la straika mpya wa Simba aliyesajiliwa kutoka Zanaco ya Zambia, Moses Phiri, alilifunga kwa mtindo wa 'tiktak' na lilifanana sana na lililofungwa na kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Msenegal Pape Sakho kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu uliopita dhidi ya Asec Mimosas kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam ambalo lilichaguliwa kuwa bao bora la michuano yote ya CAF.

Mabao yote yalikuwa ni ya kwanza kwa timu hiyo. Pape alilifunga dakika 12 likiwa ni la kwanza kabla ya Shomari Kapombe na Peter Banda kuweka mengine, ikiondoka uwanjani na ushindi wa mabao 3-1, Februari 13, mwaka huu.

Bao la juzi lilikuwa la kwanza kwenye mechi hiyo, likifungwa dakika ya 29, kabla ya John Bocco kufunga la pili.

**Yachezesha wapya watatu tu**

Kwenye mechi hiyo Simba ilichezesha wachezaji watatu tu ambao imewasajili msimu huu, huku waliobaki wakiwa ni wale wale wazoefu kwenye michuano hiyo ya kimataifa.

Wachezaji waliosajiliwa msimu huu na kupata nafasi ya kucheza ni mfungaji wa bao, Phiri, beki Mohamed Ouattara na Agustine Okrah ambaye naye aliingia kipindi cha pili.

**JE, WAJUA?**



Lionel Messi na Cristiano Ronaldo, ndio wachezaji wanaoshikilia rekodi ya kufunga hat-tricks nyingi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, kila mmoja akiwa nazo nane, huku wakifuatiwa na Robert Lewandowski mwenye sita, Karim Benzema (4) na Mario Gomez (3).





# Chombo magonjwa wanyama - binadamu chafanyiwa tathmini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHOMBO cha ufuatiliaji wa magonjwa yanayotoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu, kinatarajia kuanza kazi baada ya kufanyiwa tathmini ya kina na wataalamu ili kupunguza mlipuko wa magonjwa nchini.

Daktari wa Wanyama kutoka Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO), Dk. Henry Magwisa, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki jijini hapo alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kikao cha wadau wa afya moja.

Alisema chombo hicho kimefanyiwa tathmini na wataalamu wa magonjwa ya mifugo kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu.

"Kikao hiki kilikuwa cha kuchambua na kupitia chombo hicho imeonekana kwamba kinaweza kutufaa sana kwa sababu magonjwa ambayo yanashirikisha Wizara ya Afya na Wizara ya Mifugo, kwa Tanzania yanayopewa kipaumbele ni sita, hivyo waliitwa wataalamu wa sekta zote tatu za mazingira, mifugo na afya ili kuchambua," alisema.

Aliyataja magonjwa sita yaliyofanyiwa kazi ni kichaa cha mbwa, homa ya bonde la ufa, homa inayotokana na ndege, ugonjwa wa kimeta, homa ya malale na kitupa mimba ambayo yote hutokea kwa wanyama na binadamu.

Mtafiti na Mzoefu wa Afya Moja, Dk. Andrew Kitua, alisema nchi inaingia kwenye mfumo wa afya moja, hivyo ni muhimu kuwa na chombo hicho kutathmini mwenendo na kupima maendeleo na faida yake kwa nchi.

Alisema kazi ya chombo hicho ni kuzuia kikamilifu majanga

yasitokee kwa kujua mapema dalili zake.

Kwa mujibu wa mtafiti huyo, chombo hicho kitasaidia taarifa kupatikana wa haraka ili kudhibiti tatizo kwa muda mfupi zaidi.

Akifunga kikao hicho, Mkurugenzi Msaidizi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali Mitaa (TAMISEMI), Paulo

Chaote, aliwataka wadau kuhakikisha dhana hiyo na elimu waliojifunza inafika hadi katika ngazi ya mamlaka ya serikali za mitaa.



Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Chinyoyo jijini Dodoma, Ally Saidi (kushoto), akimpongeza Makamu Katibu Mkuu wa Kanisa la Pentecostal Holiness Association Mission Tanzania (PHAMT), Askofu Julias Bundala, baada ya kukabidhi matofali yaliyotolewa na waumini wa kanisa hilo kwa ajili ya kujenga ofisi ya mtaa huo jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wanywaji wa maziwa ghafi mikoa hii hatarini

**Na Valentine Oforo,** DODOMA

MIKOA ya Dar es Salaam na Dodoma imetajwa kuongoza kwa uuzaji wa maziwa ghafi kwa mfumo usio rasmi, hali inayohatarisha walaji kupata magonjwa.

Kwa mujibu wa kanuni za afya, maziwa yote yanayozalishwa na wafugaji ndani ya nchi, yanatakiwa kuuzwa katika vituo vya kukusanya maziwa vilivyoidhinishwa au viwanda vilivyosajiliwa na si kuuzwa moja kwa moja kwa walaji.

Msajili wa Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB), Dk. George Msalya, akizungumza na Nipashe jijini hapo jana, alisema uuzaji wa maziwa yasiyothibitishwa kitaalamu kwa matumizi, ni hatari kiafya na kiuchumi.

"Kwa mfano, wapo baadhi ya wafugaji ambao kwa kukosa uzalendo wana tabia ya kuwakamua ng'ombe wao ambao wapo kwenye dozi mbalimbali za dawa na kuyauza maziwa hayo kwa lengo tu la kupata fedha bila kujali afya za walaji," alifafanua.

Alisema Tanzania inakabiliana na wimbi la ugonjwa wa usugu wa dawa (antimicrobial resistance), shida ambayo pamoja na mambo mengine, inachochewa na unywaji wa maziwa yenye viambata vya mabaki ya dawa za mifigo.

Katika kudhibiti tatizo hilo, Dk. Msalya, alisema, TDB kwa kushirikiana na serikali inaendesha mkakati maalum wenye lengo la kutoa uelewa kwa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa nchi nzima na kubainisha kuwa kampeni hiyo kwa sasa imeanza kwa kijikita kwa kina katika majiji ya Dar es Salaam na Dodoma.

"Mkakati unalenga kuwahamasisha na kuwaelimisha wafugaji kuhusu umuhimu wa kuanza kuuza maziwa yao katika vituo rasmi ili kuondokana na matatizo mengi ya kiafya yanayoendelea kujitokeza kutokana na ukiukwaji wa sheria za uuza wa maziwa ghafi," alisema.

Alibainisha kuwa kampeni inayoendelea pia inajikita kuwaelimisha watumiaji wa maziwa nchini juu ya madhara ya kiafya wanayopata kwa kununua na kunywa maziwa moja kwa moja kutoka kwa wafugaji.

"Serikali imeweka hatua kali za kuwaadhibu wafugaji wa ng'ombe wa maziwa au maeneo ya kuuzia maziwa ghafi ambayo hayajathibitishwa kiafya kwa ajili ya matumizi ya binadamu. Adhabu hizo ni pamoja na faini za fedha na kifungo," alionya.

Alisema lengo lao ni kusimamia na kukuza sekta ndogo ya maziwa nchini, bodi hiyo imeamua kuanzia kujikita zaidi katika utoaji wa elimu badala ya kujikita katika adhabu.

"Kama baada ya kuwaelimisha wataendelea kukiuka sheria zilizowekwa, ndipo itatulazimu kuanza kuwafuatilia kupitia mifumo yetu ya kiintelijensia na kuwachukulia hatua kali," alionya.

# Mfumuko bei watajwa kiini cha ulaji usiofaa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

UTAFITI uliofanywa na Shirika la Kimataifa la Utafiti wa Masuala ya Kilimo na Chakula (CIAT), umebaini mfumuko wa bei kwenye chakula unapotokea huchangia kwa kiasi kikubwa jamii kula vyakula visivyokidhi makundi muhimu.

Mtafiti wa Masuala ya Chakula kutoka CIAT, Christine

Chege, aliyasema hayo jana wakati wa warsha ya mfumo wa kuonyesha mahitaji halisi ya chakula kwa lengo la kuboresha lishe katika nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara.

Chege alisema malengo ya kufanya utafiti huo ni pamoja na kuleta matokeo kwa serikali na taasisi husika ili kuona namna ya kufanya katika masuala ya uboreshaji lishe.

"Tumekuwa tukifanya utafiti mwingi wa masuala ya kilimo na chakula. Tumebaini pale mfumuko wa bei ya vyakula unapotokea, jamii inahifadhi fedha kwa ajili ya kununua mahindi badala ya kununua vyakula aina mbalimbali ambavyo vinaboresha afya ya mwili," alisema.

Chege alisema matokeo ya utafiti yameonyesha wananchi wanapokuwa na kipato kizuri, hula vyakula vyote ambavyo huitajika mwilini, lakini bei za vyakula zinapopanda, wengi wao hula chakula cha aina moja.

Alisema katika utafiti huo wameona pia chakula cha wananchi kinategemea bei ya mazao, akiwa na ufafanuzi kwamba bei ikipanda, Watanzania hawabadilishi chakula kwa kiwango kikubwa, hivyo kula chakula cha makundi machache.

"Bei za mahindi zikiwa juu, wananchi huweka fedha kwa ajili ya kununua mahindi badala ya vyakula vingine," alisema.

Mkurugenzi Msaidizi wa Sera na Mipango kutoka Wizara ya Kilimo, Gungu Mibavu, alisema lengo la mkutano huo ni

kutoa taaria za utafiti ambao CIAT imefanya ili ufanyiwe kazi.

Mibavu alisema matokeo mengi ya utafiti yalikuwa yakiwekwa kabatini, lakini sasa serikali kwa kushirikiana na wadau, imeanza kusambaza matokeo ya utafiti kwa wakulima ili wafahamu hatua za kuchukua na hata kufanya uamuzi sahihi katika shughuli za kilimo.

Peter Kaja kutoka Idara ya Kinga Wizara ya Afya, alisema wamepokea matokeo ya utafiti huo na kuahidi kuyafanyia kazi ili kuielimisha jamii kuhusu masuala ya lishe.





## Polisi yawapa angalizo wasiosalimisha silaha

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limewataka wananchi wote wanaomiliki silaha kinyume cha sheria, kuziwasilisha kwenye ofisi mbalimbali za serikali kabla msako haujaanza ili kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi Ulrich Matei, alitoa rai hiyo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu uwasilishaji wa silaha hizo.

Alisema usalimishaji wa silaha ulizinduliwa mkoani Dodoma hivi karibuni na unatakiwa kutelekezwa katika maeneo yote ya Tanzania na hivyo akawataka wananchi kutekeleza kwa hiari kabla jeshi hilo halijaanza hatua ya pili ambayo ni msako.

Alisema wananchi ambao watawasilisha silaha hizo kwa hiari, hawatachukuliwa hatua zozote za kisheria isipokuwa wale ambao watapatikana nazo wakati wa msako.

"Mtu anayetaka kuwasilisha silaha, anaweza kuiwasilisha katika ofisi yoyote ya serikali ama kwenye vituo vyetu vya polisi, hakuna atakayekuuliza kwamba umeitoa wapi na ulikuwa unaifanyia nini, we irejeshe tu," alisema Kamanda Matei.

Alisema wapo wananchi ambao wamekuwa wakimiliki silaha hizo kinyume cha sheria na baadhi yao wamekuwa wakizitumia kwenye matukio ya kihalifu na ndiyo sababu serikali imeamua kuja na utaratibu wa kuzirejesha.

Aliwaomba viongozi mbalimbali wa serikali kushiriki katika kuwahamasisha wananchi kuwasilisha silaha hizo ili kupunguza matukio ya uhalifu mitaani.



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Mbeya, Joseph Mwasote (kulia), akishuhudia ukusanyaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya chama hicho katika Kata ya Ndato wilayani Rungwe mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## CHADEMA yazidi kulia na tozo miamala kielektroniki

**Na Mwandishi Wetu,** RUNGWE

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Mbeya kimewataka makada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuacha kulalamikia tozo za miamala ya kielektroniki kwa madai kuwa serikali inayoongozwa na chama chao ndiyo iliyoasisi utaratibu huo. Vilevile, kimewataka watumishi wa umma ambao wamegoma kuungana na vyama vya upinzani kudai Katiba Mpya na Tume huru ya Uchaguzi, kuacha kulalamikia tozo hizo kwa madai kuwa wao ni sehemu ya wanaochelewesha mabadiliko.

Mwenyekiti wa chama hicho Mkoa wa Mbeya, Joseph Mwasote, maarufu China wa China, alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa harambee ya kuchangia ujenzi wa ofisi ya chama hicho Kata ya Ndato wilayani Rungwe.

Alidai michakato yote ya kuanzishwa kwa tozo hizo ilianzia kwenye vikao vya ndani vya CCM kabla ya kupelekwa kwenye Baraza la Mawaziri na kisha kupitishwa na Bunge ambalo pia alisema lina wabunge wengi wa CCM.

Mwasote alisema tozo hizo zinawaumiza wananchi wote bila kujali chama wanachotokea na kwamba hali hiyo wana CCM hawatakiwi kuilalamikia.

Alisema kuna haja serikali inayoongozwa na CCM ijitafakari kutokana na tozo hizo kuzua mjadala mkali kitaifa, zikipingwa na baadhi ya wadau, vikiwamo vyama vya wafanyakazi.

Aliyekuwa Diwani wa Ndato kupitia chama hicho, Paulos Zambi, alisema viongozi wa CHADEMA wamepitia katika wakati mgumu ikiwa ni pamoja na kuswekwa ndani mara kwa mara bila sababu za msingi, hali ambayo ilidhoofisha juhudi zao.

Alisema yeye ni miongoni mwa viongozi wa chama ambao waliswekwa ndani mwaka mzima akiwa ni diwani. Alisema kuwa pamoja na matatizo yote hayo, wananchi wa kata hiyo waliendelea kuwa na misimamo na hata kusaidia kulea familia yake.

Alisema kuwa akiwa gerezani, alikutana na wanachama mbalimbali wa CCM ambao pia walikuwa wanatumikia vifungo na alitumia nafasi hiyo kuwashawishi na baadaye wakakubali kuhamia CHADEMA.

"Ninawashukuru sana wanachama wenzangu kwa namna ambavyo mlituhudumia tukiwa gerezani, mlikuwa mnatuletea chakula na huduma zingine, lakini vyakula hivyo tulikuwa tunakula na wana CCM ambao tulikuwa tunatumikia nao vifungo," alisema Zambi. Aliyekuwa Mwenyekiti wa CHADEMA Mbeya Mjini, John Mwambigija, aliwataka wanachama wa chama hicho kuendelea na harakati za ukombozi ili kuondoa kero mbalimbali ambazo zimekuwa zikiwakabili ikiwamo uanzishaji wa tozo.

Mwambigija alisema chama hicho ndicho kimekuwa kikisaidia kuleta mabadiliko ya vitu mbalimbali nchini, hivyo akawataka wananchi kuendelea kukiamini.

Hata hivyo, siku nne zilizopita, Katibu wa NEC Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, ikiwa ni siku moja baada ya Kamati Kuu ya CCM kuketi, alisema kikao hicho kimetoa maelekezo sita kwa serikali ikiwamo kutazama hali halisi na kuchukua hatua stahiki kuhusu utozaji wake wa kodi.

Shaka alisema hatua ambazo chama hicho kimetaka zichukuliwe ni pamoja na kuzingatia maoni na ushauri wa wananchi kuhusu tozo hizo.

## Wakaguzi ubora wapewa darasa ukaguzi mipakani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KATIBU Tawala Msaidizi Viwanda na Biashara wa Mkoa wa Mbeya amewataka wakaguzi wa ubora wa bidhaa wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) wanaofanya kazi kwenye maeneo ya mipakani, kufanya kazi kwa kuzingatia sheria na kuwa waadilifu ili kuwahudumia vizuri wananchi na kukuza biashara.

Mwajabu Nyamkomola alitoa agizo hilo ijini Mbeya juzi alipofungua mafunzo ya ukaguzi kwa maofisa biashara na maofisa afya wa halmashauri za mkoa huo.

Mafunzo hayo yanatolewa na TBS kwa maofisa hao kwa lengo la kuboresha shughuli za ukaguzi wa ubora wa bidhaa mbalimbali zikiwamo zinazoingizwa nchini zikitoka nchi jirani.

Nyamkomola alisema kazi ya ukaguzi wa bidhaa inahitaji uadilifu wa hali ya juu kutokana na kwamba inahusisha maisha ya watu moja kwa moja, hivyo uadilifu ukiwa mdogo, uhatarisha maisha ya watu.

Alisema tatizo kubwa lililoko maeneo ya halmashauri ambazo zipo mipakani, ni uingizaji wa bidhaa hafifu na kwamba kwa Mkoa wa Mbeya tatizo kubwa ni uingizaji wa vipodozi vyenye viambata sumu.

"Ninawaomba mhakikishe mnafanya kazi yenu kwa uadilifu mkubwa, zingatieni sheria na miongozo ya kazi zenu za ukaguzi, kule mpakani hakikisheni mnakagua vizuri bidhaa ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi," aliagiza.

Kaibu Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Ashura Katunzi, alisema mafunzo hayo yanatolewa nchi nzima kwa maofisa mbalimbali ambao wanashirikiana nao kwenye shughuli za ukaguzi, hasa baada ya shirika hilo kukabidhiwa majukumu ambayo awali yalikuwa yanatekelezwa na iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA).

Alisema kabla ya kwenda Mbeya, walianzia Mkoa wa Njombe, lengo la mafunzo hayo likiwa kuboresha shughuli za ukaguzi ambazo zimekuwa zikifanyika kila siku nchini, hasa kwenye maeneo ya uzalishaji na ya biashara.

Alisema maofisa afya na maofisa biashara kwa sasa ndiyo wanaofanya kazi ya ukaguzi kwa kushirikiana na maofisa wa TBS na hivyo wanafundishwa taratibu za ukaguzi, sheria za ukaguzi na vitu ambavyo wanatakiwa kukagua.

Vilevile, alisema maofisa hao wanafundishwa namna ya kutambua bidhaa zenye ubora na zenye ubora hafifu pamoja na hatua za kisheria zinazotakiwa kuchukuliwa wanapobaini bidhaa hizo sokoni.

"Ninyi maofisa hamtakiwi kufanya kazi kwa nguvu kama walivyo polisi, zipo taratibu maalum ambazo mnatakiwa kuzingatia ili ukaguzi ufanyike kisheria na muwasaidie wananchi," aliagiza.

Meneja wa TBS Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Abel Mwakasonda, aliwataka maofisa hao kuwa makini wakati wa kupewa mafunzo hayo ili wajue mipaka ya kazi yao na watoa huduma kwa wananchi hasa kwenye shughuli za ukaguzi.

Alisema maofisa hao baada ya mafunzo hayo watakasimishwa baadhi ya majukumu ya ukaguzi kwa maelezo kuwa wao ndiyo wapo jirani zaidi na wananchi.





# Dk. Mwinyi aagiza madaktari bingwa wapelekwe wilayani

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Serikali ya Zanzibar ikikamilisha ujenzi wa hospitali za wilaya zote Unguja na Pemba, hospitali ya mkoa na ya rufani, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameagiza hospitali hizo lazima ziwe na madaktari bingwa.

Akizungumza Ikulu Zanzibar wakati wa kuwaaga madaktari 21 kutoka China waliokuwa wakitoa huduma visiwani humo, Rais Dk. Mwinyi aliiomba Serikali ya China kuleta madaktari bingwa ili kwenda sambamba na dhamira ya serikali yake katika kuboresha huduma za afya. Alisema hospitali hizo zitakapokamilika zitakuwa na vifaa na maeneo yote muhimu katika utoaji wa huduma, hivyo timu ijayo ya madaktari kutoka China itakuwa katika mazingira bora zaidi ya kufanyia kazi.

Dk. Mwinyi aliipongeza timu hiyo ya madaktari kwa kazi kubwa iliyofanya kwa kusaidia utoaji wa huduma za kinga, tiba, dawa na vifaa huduma za kinga na kufanya upasuaji wa magonjwa mbalimbali.

Aliwashukuru madaktari hao kwa kutoa mafunzo na kuwajengea uzoefu madaktari wazalendo, wauguzi na wafanyakazi wa sekta ya afya. Waziri wa Afya, Ahmeid Nassor, alipongeza uhusiano na ushirikiano wa muda mrefu uliopo kati ya Serikali ya Watu China na Tanzania.

Alikumbusha kuwa tangu mwaka 1964 kumekuwa na utaratibu kwa China kutuma timu ya madaktari nchini kila mwaka na akatumia fursa hiyo kuipongeza timu hiyo kwa kazi kubwa waliyofanya katika kutoa huduma bora kwa jamii.

"Timu hiyo haikuishia kufanya kazi katika hospitali kubwa pekee, bali ilifika hadi katika vituo vya afya vilivyoko vijijini, hatua hii ilibainisha ari kubwa waliyonayo madaktari hawa katika utendaji wao wa kazi uliotukuka," alipongeza.

Waziri huyo alisema utendaji wao umeamsha ari kubwa na utasaidia kuwajengea uzoefu madaktari wazalendo. Madaktari hao kutoka China walisema utaratibu wa China kutuma madaktari Zanzibar uliasisiwa mwaka 1964 kwa lengo la kujenga ushirikiano katika kutatua utatuzi wa shida za huduma za afya, ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kuendeleza ushirikiano kati ya China na Zanzibar.



Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, akizungumza na walimu wakuu wa shule za sekondari, msingi, maandalizi na wenyeviti wa kamati za shule wa Mkoa wa Kusini Unguja katika ukumbi wa mikutano wa Dk. Shein Tunguu Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Makamu Rais aushtukia uteuzi wa walimu wakuu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdullah, amesema Serikali ya Zanzibar imeutaka uongozi wa Wizara ya Elimu kuangalia upya vigezo vya upatikanaji wa walimu wakuu kulingana na sifa zilizowekwa kisheria ili kuirejeshea heshima sekta ya elimu Zanzibar.

Amesema kuna baadhi ya walimu wakuu hawana sifa ya kushika wadhifa huo, akiagiza hatua zichukuliwe kurekebisha dosari hiyo.

Akizungumza jana mjini Zanzibar katika mkutano na wakuu wa shule za sekondari, msingi, maandalizi na wenyeviti wa kamati za shule Mkoa wa Kusini Unguja, Hemed alisema serikali imeamua kuipa kipaumbele sekta ya elimu kulingana na mahitaji ili kuzalisha wataalamu bora.

Makamu wa Rais alisema wizara inapaswa kuhakikisha inawasimamia ipasavyo walimu wakuu wote kwa lengo la kuboresha elimu na kuongeza ufaulu ili kupata viongozi bora na wataalamu wa baadaye.

Hemed pia aliwataka walimu wakuu kuwajibika, kufuatilia na kusimamia vyema walimu walio chini yao pamoja na wanafunzi ili kujenga nidhamu.

Aliagiza kila mwalimu mkuu lazima asimamie kwa kufuata misingi ya sheria, haki na wajibu ili kufanikisha azma ya serikali ya kutatua shida zinazoikabili elimu kwa mikoa yote ukiwamo wa Kusini Unguja.

"Ni lazima kuhakikisha tunasonga mbele kwenye ufaulu wa wanafunzi na serikali imedhamiria kuleta mapinduzi makubwa kwenye sekta ya elimu kwa mikoa yote," alisema.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhamed Mussa, alisema wizara imejipanga kufungua kidato cha tano na sita katika Shule ya Hasnuu Makame ili kutatua kero zinazowakabili wanafunzi wanaofaulu, kufuata elimu hiyo umbali mrefu.

Waziri Leila alisema wizara itahakikisha inazitatua kero zote zinazowakabili walimu ili malengo ya serikali ya kutoa elimu bora kwa wananchi na kupata wataalamu bora yafikiwe.

Baadhi ya walimu wakuu na wenyeviti wa shule za Mkoa wa Kusini Unguja waliomba serikali kutatua kero zote zinazowakabili walimu wa mkoa huo ikiwamo uhaba wa walimu, uhaba wa vitendea kazi na kupatiwa stahiki zao ili kuleta ufanisi.

# Bei mafuta ya ndege yashuka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma ya Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), imetangaza bei mpya za mafuta zilizoanza kutumika kwa mwezi huu, bei ya mafuta ya ndege ikishuka.

Bei ya mafuta hayo kwa mwezi wa Agosti ilikuwa Sh. 3,147 na kwa mwezi huu lita inauzwa kwa Sh. 2,681.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari ofisini kwake Maisara Mjini Zanzibar juzi, Meneja Kitengo cha Uhusiano wa ZURA, Mbarak Hassan, alisema kwa mwezi huu bei ya mafuta ya petroli ni Sh. 2,980, dizeli Sh. 2,990 na mafuta ya taa Sh. 2,921, sawa na bei ya mwezi wa Agosti.

Alisema hatua hiyo inatokana na serikali kuendelea kufidia bei ya nishati hiyo nchini pamoja na nishati hiyo kushuka katika soko la dunia.

Alibainisha kuwa kwa miezi mitatu iliyopita kuanzia Juni hadi Agosti, serikali ilifidia jumla ya Sh. bilioni 13.7, akifafanua kuwa kwa mwezi Juni fidia ilikuwa Sh. bilioni 2.4 na mwezi Julai Sh. bilioni 2.6.

Alisema kuwa mwezi Agosti serikali ilifidia Sh. bilioni 8.7 kwa bei za mafuta, akimpongeza Rais wa Zanzibar kwa kuendelea kuwajali wananchi katika kufidia bei hizo.

Meneja huyo alisema wananchi wafahamu kuwa ZURA inapanga bei kwa kuzingatia mambo mbalimbali ikiwamo wastani wa mwenendo wa mabadiliko ya bei za mafuta na gharama za uingizaji mafuta katika Bandari za Dar es Salaam na Tanga.

Meneja huyo aliwataka wananchi kununua mafuta katika vituo halali vya mafuta na kudai risiti wanapopata huduma hiyo ili kuiwezesha serikali kupata mapato yake.

# Maktaba zinavyosaidia wanafunzi kuleta ushindani

**Na Julieth Mkireri**

SHULE zenye maktaba zimegundulika wanafunzi wake kuwa na uwezo wa kujieleza na kuleta ushindani tofauti na zisizokuwa na huduma hiyo.

Aidha, maktaba zinasaidia wanafunzi kutokariri masomo na kuleta ushindani wa wenyewe kwa wenyewe wanapojifunza.

Mwalimu wa Shule ya Msingi Kwamgwe, Handeni mkoani Tanga, Zamiru Salehe, alisema hayo alipokuwa akizungumza kwa njia ya mtandao kwenye kongamano la maadhimisho ya siku ya usomaji lililoandaliwa na Shirika la Room to Read na kufanyika jijini Dar es Salaam.

Wadau na walimu katika shule tofauti walielezea umuhimu wa maktaba shuleni kwa ajili ya wanafunzi kujisomea na kujifunza.

Mwalimu Salehe alisema, wanafunzi wanapata fursa ya kuazima vitabu kutoka maktaba na kwenda kujisomea nyumbani na wengine wakitumia muda wa mapumziko kukaa maktaba kujisomea jambo ambalo limeleta mabadiliko kimasomo.

Naye Mwalimu Rose Mkombozi kutoka Tanga, alisema kupitia maktaba, nidhamu shuleni imedumishwa na wanafunzi kwa kujisomea vitabu mbalimbali vinavyowaelimisha.

"Wanafunzi wa kike wamekuwa wakishirikishana namna ya kujitambua, pia ufaulu umekua hii imetokana na maktaba tuliyopata katika shule yetu," alisema Rose.

Mwalimu Ahmed Shehe alisema kutokana na kuwapo kwa maktaba katika shule kumechangia ongezeko la wanafunzi wanaoandikishwa na kupunguza utoro baada ya wanafunzi kuhamasishana kusoma muda wa mapumziko na kuazima vitabu.

Ofisa Elimu Halmashauri ya Ubungo, Joseph Mabeyo akizungumza katika kongamano hilo, alisema amepata mradi wa makataba katika shule 28 kati ya 66 za halmashauri yake.

Mabeyo alisema shule 21 katika awamu ya kwanza zitanufaika na maktaba za makontena na zilizopata fedha ni saba.

Mkurugenzi wa Room to Read, Juvenalius Kuruletera alisema shirika hilo limejikita zaidi kufanya kazi na jamii na hadi sasa wamefikisha maktaba katika baadhi ya shule za msingi nchini.

Alisema wanafanya hivyo ili kuwezesha wanafunzi wengi kujua kusoma na kuandika na kujifunza mambo mbalimbali.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni jijini Dar es Salaam, Kamishana Msaidizi wa Jeshi la Polisi ACP Mtatiro Kitinkwi, akizungumza na viongozi wa serikali za mtaa Mabwepande jana, kuhusu ulinzi na usalama. Kulia ni Kamanda wa Polisi Mabwepande OCD Sp. Colle Senkondo na kushoto ni Mwenyekiti wa Wenyeviti Wilaya ya Kinondoni, Razalous. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# CCM Masasi wafundwa maadili uongozi

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

VIONGOZI na wanachama wa Mkutano Mkuu wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Mpeta, Masasi wamepatiwa mafunzo elekezi ya uongozi bora ili kutambua vyema majukumu ya kazi zao na kuheshimu miiko ya chama.

Mafunzo hayo yametolewa jana mjini hapo na Katibu wa Umoja wa Vijana (UVCCM), Mkoa wa Mtwara, Julius Simalenga, kupitia mkutano mkuu wa chama hicho.

Simalenga alisema ili kufanya kazi za chama hicho kila kiongozi kuanzia ngazi ya chini, wilaya na taifa lazima atambue majukumu yake kikamilifu na mipaka yake ya kazi.

Alisema chama kinafanyakazi kwa kufuata kanuni na miongozo iliyojiwekea katika kutekekeza majukumu yake ikiwamo ya kuishauri serikali iweze kuwatumikia wananchi wake na kwamba viongozi lazima watambue majukumu yao ipasavyo.

Alisema uongozi ni dhamana na kila mmoja lazima atambue majukumu yake na mipaka ya kazi anayoifanya. Hakuna sababu ya kiongozi kutengeneza makundi katika kutimiza majukumu yake.

Alimtaka kila kiongozi kutambua kwamba anatumia nafasi yake ya uongozi kwa kufuata sheria na kanuni za nchi pamoja na za chama kilichomweka madarakani.

Simalenga alisema anafurahi kuona Mkoa wa Mtwara una vijana wengi walioteuliwa kushika nafasi za uongozi na ari ya kufanya kazi.

Alisema hapaswi kuwa na ubinafsi anapoongoza, aheshimu kila mmoja na kuwaheshimu viongozi wa ngazi ya juu kuanzia ndani ya chama na serikali.

Naye mshiriki mafunzo hayo, Issa Ismaily, alisema mafunzo yatamsaidia kufanyakazi kwa kuwa ameweza kufahamu vyema misingi na mipaka ya kazi zake na kwamba atazingatia miongozo yote ya kazi.

# SHIVYAWATA yaiomba serikali wataalamu lugha za alama

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SHIRIKISHO la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA), limeomba serikali kuajiri wataalamu wa lugha za alama katika taasisi za umma ili kupunguza vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanachama wao.

Taasisi hizo ni pamoja na Jeshi la Polisi kitengo cha dawati la jinsia, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), mahakama, hospitali, ustawi wa jamii pamoja na idara za maendeleo ya jamii katika halmashauri zote nchini.

Katibu wa SHIVYAWATA Wilaya ya Kahama, Masunga Robert, aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na vyombo vya habari ofisini kwake kuhusu namna wanavyoshirikiana na taasisi mbalimbali za serikali kutokomeza vitendo vya ukatili kwa viziwi.

Alisema viziwi katika jamii wanafanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia na kushindwa kutoa taarifa kwenye mamlaka husika kwa hatua zaidi za kisheria kwa sababu ya ukosefu wa wataalamu wa lugha za alama na kubaki na majeraha katika mioyo yao.

Alipendekeza ili kuondoa vitendo hivyo ni vyema serikali ikaajiri wataalamu hao katika hizo za umma.

Robart aliwataka viziwi wanapofika katika ofisi zao kutoa malalamiko yao wahakikishe wanapata msaada wa SHIVYAWATA kwa ajili ya kupatiwa wataalamu wa kutafsiri.

Kwa upande wake, Jamillah Saidi, alisema viziwi wanafanyiwa vitendo viovu kwenye jamii na hawana sehemu ya kupeleka malalamiko yao.

Alisema ndugu yake ni kiziwi na amejifunza kuzungumza naye kwa njia ya vitendo tangu utoto wake mpaka sasa ni mtu mzima na kwamba linapotokea jambo ndani ya jamii ni rahisi ndugu yake kueleza na kupatiwa msaada kwa kuwa anahaki kama walivyo watu wengine.

Kwa upande wake, Edward Charles alisema kipindi cha nyuma waliwahi kupewa elimu ya namna ya kuzungumza na wenzao kwa kutumia lugha za alama na wanaelewana hao vizuri na kushauri vyombo vya umma visisite kuwatumia.



## HABARI KIMATAIFA

# Russia yaondoa majeshi yake Kharkiv

**KYIV,** UKRAINE

WAKATI Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelenskiy, akisema jeshi la taifa lake limefanikiwa kulikomboa eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 2,000, Russia imetangaza kuyaondoa majeshi yake mashariki mwa Kharkiv.

Katika taarifa ya Zelensky aliyoitoa jana kwa njia ya video, alisema hatua ya kulikomboa eneo hilo inatokana na kufanikiwa kwa operesheni yake ya kukabiliana na vikosi vya Russsia ambayo iliianza mwezi huu.

Awali mwishoni kwa wiki iliyopita Rais Zelensky, alisema vikosi vyake vimeweza kuyadhibiti maeneo ya makazi zaidi ya 30 katika mkoa huo wa Kharkiv.

Wizara ya Ulinzi ya Russia pia ilitangaza kuyaondoa majeshi yake katika maeneo mawili ya mashariki mwa Ukraine katika mkoa wa Kharkiv, eneo ambalo vikosi vya Ukraine vimekuwa vikipiga hatua muhimu ya kusonga mbele katika makabiliano yake na Russia tangu juma lililopita.

**Aidha, mwishoni mwa wiki iliyopita Wizara ya Ulinzi ya Uingereza ilisema kwamba inaamini wanajeshi wa Ukraine wamesonga mbele hadi kilomita 50 kusini mwa Kharkiv.**

Taarifa hizo zilitolewa baada ya siku kadhaa ya kusonga mbele kwa vikosi vya Ukraine kwa upande wa kusini mwa Kharkiv, katika mji huo ambao ni wa pili kwa ukubwa nchini Ukraine, katika kile kinachotazamwa kama mafanikio makubwa katika uwanja wa vita, tangu vilipozuia jaribio la Russia kuuteka mji mkuu wa Kyiv, mwanzoni mwa vita iliyodumu karibu miezi saba sasa.

**SABABU RUSSIA KUJIONDOA**

Msemaji wa Wizara ya Ulinzi wa Ukraine, Igor Konashenkov, alisema vikosi vya Russia vinarejea kwenda kujipanga upya katika eneo la Balakliya na Izyum, mashariki mwa mkoa wa Donetsk.

Ilielezwa kuwa Izyum ilikuwa kambi kubwa ya vikosi vya Russia katika mkoa wa Kharkiv, na mwanzoni mwa wiki iliyopita video za mitandao ya kijamii zilionyesha wakazi wa Balaklia wakifurahia na kuwashangilia wanajeshi wa Ukraine waliokuwa wakiingia katika viunga vya mji huo.

Msemaji Konashenkov alieleza kwamba hatua ya Russia imetokana na mpango wa kufanikisha malengo kadhaa, katika operesheni maalumu ya kijeshi yenye lengo la kuikomboa Donbas, mmoja kati ya mikoa ya Ukraine ambayo Russia imeitangaza kuwa huru.

Alisema sababu ya kujiondoa ili kutoa zingatio kwa eneo la Donetsk ni sawa na ile iliyoipa uhalali Russia katika hatua ya kuyarejesha nyuma majeshi yake kutoka katika maeneo ya karibu na Kyiv, mwanzoni mwa mwaka huu pale iliposhindwa kudhibiti mji mkuu huo.

Aidha, mwishoni mwa wiki iliyopita Wizara ya Ulinzi ya Uingereza ilisema kwamba inaamini wanajeshi wa Ukraine wamesonga mbele hadi kilomita 50 kusini mwa Kharkiv, na kuvisukuma vikosi vya Russia karibu na eneo la Izyum.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa kilichojitokeza kimevistusha vikosi vya Russia, ambapo licha ya mafanikio ya Ukraine, Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken na Mkuu wa Jumuiya ya Kujihami ya (NATO) walionya kwamba vita hivyo vinaweza kuendelea kwa miezi.

Blinken alisema mzozo huo unaingia katika kipindi kigumu na hivyo kuwataka waungaji mkono wa Ukraine ambayo ni mataifa ya Magharibi mwa Ukraine kuendelea kuiunga mkono hata katika kile alichokiita kipindi kigumu cha msimu wa baridi. **DW**

## Mfalme Charles asifu utawala wa Malkia

**LONDON,** UINGEREZA

MFALME Charles III baada ya kutangazwa rasmi mrithi wa malkia ameupongeza utawala wa Malkia Elizabeth kwamba ulikuwa usio na mfano.

Mfalme Charles III alipokea wadhifa huo baada ya kifo cha mama yake hayati Malkia Elizabeth II, ambapo mkutano wa baraza maalum ulimthibitisha rasmi mwishoni mwa wiki iliyopita.

Akizungumza mbele ya baraza lililomtangaza Mfalme Charles, alisema kifo cha mama yake ni pengo lisilojazika.

Wakati huo huo, mawaziri wakuu katika bunge la wawakilishi, akiwamo Waziri Mkuu Liz Truss walikula kiapo mbele ya mfalme mpya Charles, ambapo kikao rasmi cha kihistoria kilithibitisha jukumu lake Septemba 10.

Baraza la kumtangaza rasmi mfalme, linajumuisha wanasiasa wakuu, majaji na maofisa wengine walimtangaza rasmi kama mfalme, huku ikielezwa kuwa ni mara ya kwanza hafla hiyo kuonyeshwa kwenye televisheni. **BBC**





Wanajeshi wa Russia wakiondoka katika mji ulioko mashariki mwa Ukraine Kharkiv, baada ya vita iliyodumu kwa takribani miezi saba. **PICHA: MTANDAO**

# Uganda kuilipa DRC fidia dola mil.325

**KINSHASA,** DRC

WAZIRI wa Sheria wa Jamhuri ya Kidemkorasia ya Kongo (DRC), Rose Mutombo, amesema Uganda imeanza kuilipa Kinshasa fidia ya dola milioni 65 kati ya 325 kama ilivyoamriwa na Mahakama ya Sheria ya Kimataifa ICJ.

Kwa mujibu wa maofisa wa Kinshasa waliozungumza mwishoni mwa wiki iliyopita, Waziri wa Sheria Rose, aliliarifu Baraza la Mawaziri siku ya Ijumaa kuwa Uganda imeanza kulipa fidia na riba baada ya ICJ kuikuta na hatia ya uvamizi wa mashariki mwa Congo miaka 20 iliyopita.

Waziri huyo aliliambia baraza kwamba kulingana na makubaliano Uganda itailipa Congo fedha zote kwa awamu tano ikiwa ni dola milioni 65 kila mwaka, ambapo malipo ya kwanza yalishatolewa Septemba mosi, mwaka huu.

Baada ya mivutano ya kisheria ya muda mrefu, Mahakama ya Sheria ya Kimataifa, chombo kikuu cha sheria cha Umoja wa Mataifa, Februari 10 mwaka huu, kilifikia uamuzi wa kuitaka Kampala kuilipa Kinshasa dola milioni 325 kwa kuivamia Congo wakati wa vita vyake vya pili, vilivyotokea kati ya 1998 hadi 2003.

Inaelezwa kuwa kiwango hicho cha fedha ni kidogo kulingana na dola bilioni 11 ambazo DRC imekua ikidai, huku ikidaiwa kuwa Uganda imeichukulia hukumu hiyo haikuwa ya haki, na kwamba wamesikitishwa na uamuzi uliochukuliwa wakati nchi hizo mbili zilikuwa zinaendelea kuimarisha uhusiano kati yao.

Aidha, Waziri wa Sheria aliliambia baraza la mawaziri kwamba fedha zilizolipwa na Uganda zitawekwa katika akaunti ya muda ya wizara ya sheria, katika benki ya Congo, na kwamba fedha hizo haziwezi kutumiwa hadi zilipwe kwa ukamilifu na kutumiwa kwa ajili ya mfuko maalum kuwalipa fidia waathirika.

Ilipokuwa inatoa uamuzi wake mahakama ya ICJ ilieleza kwamba kati ya dola milioni 325, ni dola 225 zitakazotumiwa kuzilipa familia za waliouawa, na dola milioni 40 kulipa hasara za mali na milioni 60 fidia kwa maliasili iliyopotea.

HABARI MICHEZO

# JOTO LAPANDA NMB MARATHON UKAGUZI WA NJIA UKIFANA DAR

Na Mwandishi Wetu

JOTO la Mbio za Hisani za NMB Marathon 2022 zinazolenga kukusanya kiasi cha Sh. milioni 600 kusaidia matibabu ya kinamama wenye fistula nchini wanaotibiwa katika Hospitali ya CCBRT, limezidi kupanda baada ya kufanyika kwa ufanisi ukaguzi wa njia zitakazotumika 'routes check' hapo Septemba 24.

**Huu ni msimu wa pili wa mbio] hizo, ambazo zilianza kutimua vumbi mwaka jana, lengo likiwa ni kukusanya Sh. bilioni moja katika kipindi cha miaka minne, lakini mafanikio yaliyowezesha kukusanya Sh. milioni 400 badala ya milioni 250, yakaisukuma Benki ya NMB inayoandaa kupanga kukamilisha Sh. milioni 600 zilizobaki mwaka huu.**

Ukaguzi wa njia zitakazotumiwa na wakimbiaji wa mbio hizo, ulifanyika Jumamosi ukihusisha mbio za kilomita tano, 10 na 21, zilizoanzia na kuishia Leaders Club Kinondoni, Dar es Salaam, mahali ambako ndiko zitakorindima mbio zenyewe hapo Septemba 24, mwaka huu ambako Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, atakuwa mgeni rasmi.

Akizungumza baada ya ukaguzi huo, Mratibu wa mbio hizo, Suleiman Nyambui, alisema majaribio ya ukaguzi wa njia yamekuwa na mafanikio kwa washiriki na kwamba matumaini yao kama waratibu ni kwamba, wanariadha watakaojisajili kushiriki mbio hizo watafurahia kutokana na maandalizi yaliyoko.

"Kumekuwa na mafanikio makubwa katika ukaguzi huu, na washiriki wamerídhishwa sana na alama za barabarani zilizoko kila kona ya njia na vituo vya kupokelea maji ya kunywa.

"Changamoto ya hizi mbio mara nyingi huwa ni alama katika njia za kukimbilia kwa washiriki wa umbali tofauti, ila NMB Marathon hakuna atakayepotea, labda mtu aamue mwenyewe kujipoteza," alisema Nyambui huku akiwataja Emmanuel Giniki na Failuna Matanga kuwa miongoni mwa watakaoshiriki.

Kwa upande wa Ofisa Mkuu wa Rasilimali Watu wa Benki ya NMB, Emmanuel Akonaay, alisema ukaguzi huo ulioshirikisha zaidi ya wakimbiaji 100, umefanyika kwa ufanisi mkubwa, huku akitoa wito kwa Watanzania kuendelea kujisajili katika matawi ya benki hiyo na mtandaoni ili kufanikisha ukusanyaji wa Sh. milioni 600.

"Mbio hizi ni mwendelezo wa zile za mwaka jana. Tuliweka lengo la kukusanya Sh. bilioni moja, lakini mwaka wa kwanza tu tukapata Sh. milioni 400, ufanisi uliotusukuma kuweka lengo la kukusanya Sh. milioni 600 mwaka huu ili kumaliza lengo la miaka minne katika kipindi cha miaka miwili ya kwanza," alisema Akonaay.

Kiongozi mwanzilishi wa Klabu ya Mbio za Taratibu cha EFM, Maulid Kitenge, aliisifu NMB kwa uwekezaji katika maandalizi ya mbio hizo na kwamba ana uhakika wanariadha watakaoshiriki hapo Septemba 24 watafurahia kuwa sehemu ya tukio hilo linaloenda kurejesha tabasamu kwa kinamama wenye fistula.



Ofisa Mkuu wa Rasilimali Watu Benki ya NMB, Emmanuel Akonaay (katikati), akiwaongoza washiriki wa mbio za kilomita 10 wakati wa ukaguzi wa njia za kukimbilia 'route check' ya NMB Marathon, zilizoanzia na kuishia viwanja vya Leaders Club vilivyoko Kinondoni, Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. NMB Marathon 2022, zitakazofanyika Septemba 24, mwaka huu viwanjani hapo, zinatarajiwa kukusanya Sh. milioni 600 za kusaidia matibabu ya kinamama wenye fistula katika Hospitali ya CCBRT. **MPIGAPICHA WETU**

## Uwanja wa Kikapu Ilala wakabidhiwa

Na Faustine Feliciane

MKUU wa Wilaya ya Ilala Ng'wilabuzu Ludigija, amesema kukamilika kwa ukarabati wa uwanja wa mpira wa kikapu wa Spider katika Manispaa yake kutatoa fursa ya vijana wengi kucheza mchezo huo na kuongeza hamasa ya michezo wilayani hapo.

Ludigija ameyazungumza hayo mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa uwanja huo, uliofanyiwa ukarabati mkubwa na Kampuni ya Moet Hennessy kwa ushirikiano na NBA Afrika.

Ludigija alisema Wilaya ya Ilala ni kitovu cha michezo katika mkoa wa Dar es Salaam, hivyo uwapo wa uwanja huo uliokarabatiwa, kwa kiasi kikubwa umezidi kuiongezea sifa Ilala.

"Tunafahamu wote kuwa michezo kwa sasa ni ajira, kuwapo kwa viwanja vingi vya michezo mbalimbali kunatoa fursa kwa vijana wengi kujikita kwenye michezo, lakini pia haya yanayofanywa pia ni kuunga mkono juhudi za Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan ambaye ameweka wazi mapenzi yake kwenye michezo ," alisema Lubigija.

Kwa upande wa Meneja Masoko wa Kampuni ya Moet Hennesy iliyoshirikiana na NBA Afrika kukarabati uwanja huo, Janet Mwalilino, alisema mchakato wa ukarabati wa uwanja huo ulianza muda mrefu baada ya kukutana na NBA Afrika na wanafurahi kuukabidhi baada ya ukarabati mkubwa walioufanya.

"Huu ni uwanja wa kwanza Afrika Mashariki, tumefanya hivi kwa kushirikiana na NBA Afrika katika nchi za Nigeria, Ghana na Cameroon lakini kwa Afrika Mashariki, huu ndio uwanja wa kwanza," alisema Janet.

Aidha, alisema baadhi ya vitu walivyoviongeza kwenye uwanja huo ni taa ili kuwawezesha wachezaji kucheza muda wanaoutaka wao hata usiku.

Mwenyekiti wa Klabu ya Spider, Lwaga Nikipula, alisema kwa sasa wanajipanga kutafuta mbinu ya kujenga majengo ya kubadilishia nguo.

# Shabiki Simba ashinda mamilioni ya M-Bet

Na Mwandishi Wetu

SHABIKI wa Klabu ya Simba anayeishi mkoani Arusha, Joseph Marwa, ameshinda Sh. 60,321,350 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 za ligi mbalimbali duniani kupitia mchezo wa Perfect 12 wa Kampuni ya M-Bet.

Marwa ambaye ni mjasiriamali, alisema awali hakuwa na imani na michezo ya kubashiri kabisa mpaka alipofuatwa kukopwa fedha ya nauli na mmoja wa washindi Kampuni ya M-bet.

Alisema kuwa mshindi huyo alimfuata kumkopa nauli ya kwenda Dar es Salaam na kuahidi angemrudishiwa baada ya kupokea fedha alizoshinda.

Alifafanua kuwa kwa vile alikua pamoja na kumfahamu mshindi huyo, bado alikuwa anasita kumkopesha kwani kipindi hicho hakuwa na imani na michezo ya kubashiri.

"Nilimpa Sh. 150,000 mshindi na rafiki yake ambao walikuja Dar es Salaam kufuata fedha hizo. Sikuwafuatilia kabisa kwa sababu walikuwa vijana ninaowafahamu, lakini baada ya kurejea, kijana alinirejeshea fedha yangu na kwa kuongeza Sh. 50,000 zaidi.

"Sikuamini kabisa na kuanza kumhoji maswali kadhaa na baadaye kumwomba anifundishe kuweka mkeka. Alifanya hivyo na siku ya kwanza tu tokea kuanza kubashiri, nilishinda 800,000 na zaidi ambazo nilitumiwa kwenye simu," Marwa alisema.

"Tokea hapo nikaanza kubashiri na M-Bet na kushinda fedha mbalimbali kabla ya kuibuka mshindi katika Jackpot."

Marwa pia aliwapa rai vijana wenye umri kuanzia miaka 18 kuacha kutumia Sh. 1,000 kununua sigara na kuvuta wakati wanaweza kuzitumia fedha hiyo kubashiri na M-Bet na kujishindia mamilioni ya fedha kama yeye.

Mkurugenzi wa Masoko wa M-Bet, Allen Mushi, alisema Marwa anakuwa mmoja wa wanachama wa nyumba yao ya mabingwa kwani ni mshindi wa tisa wa Jackpo tokea kuanza mwaka huu.

"Tunaposema M-Bet ni nyumba ya mabingwa, tunakuwa na maana maalum, mpaka sasa tumewazadia mamilioni washindi nane na wameweza kubadili maisha yao," alisema Mushi.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SILVA KUWANIWA JANUARI

BARCELONA itajaribu tena kumsajili kiungo wa Manchester City, Bernardo Silva mwenye umri wa miaka 28 Januari. ***(Sport, via Mirror Online)***

### CAICEDO MKATABA MPYA

KLABU ya Brighton and Hove Albion ipo tayari kujadiliana na Moises Caicedo kuhusu mkataba mpya, huku Manchester United, Liverpool na Arsenal zikionyesha nia ya kumtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 kutoka Ecuador. ***(Sunday Mirror)***

### WIND AITAKA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Wolfsburg na Denmark, Jonas Wind mwenye umri wa miaka 23, amesema kuhamia Arsenal itakuwa ni "ndoto". ***(Bulinews.com, via Mail Online)***

### DEST ANGETUA UNITED

KLABU ya Manchester United ingeweza kumsajili mlinzi wa Barcelona na Marekani, Sergino Dest mwenye umri wa miaka 21, kutoka Barcelona, lakini bodi ilikataa. ***(The Athletic)***

### ICARDI KULIPWA NA PSG

KLABU ya Paris St-Germain inapanga kulipa asilimia 90 ya mshahara wa Mauro Icardi wakati mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, akiwa kwa mkopo kule Galatasaray msimu huu. ***(RMC, via Mirror Online)***

### RAPHINHA NA NEYMAR

FOWADI wa zamani wa Leeds United, Raphinha mwenye umri wa miaka 25, amesema uamuzi wake wa kuikataa Chelsea na kuhamia Barcelona ulitokana na ushauri wa Neymar. ***(La Vanguardia, via Metro)***

### LEEDS YAMPOTEZEA DIENG

LEEDS United haina mpango wa kufufua mpango wao wa kutaka kumsajili Bamba Dieng mwenye umri wa miaka 22 kutoka Marseille, baada ya kumkosa kipindi cha majira ya joto kilichopita. ***(Express Online)***

### TEBAS AISHUTUMU PSG

RAIS wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Javier Tebas, ameishutumu Paris St-Germain na Kylian Mbappe baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, kukataa kuhamia Hispania. ***(Mirror Online)***

### FELIX HAJUI CHOCHOTE

FOWADI wa Atletico Madrid na Ureno, Joao Felix mwenye umri wa miaka 22, amesema hajui chochote kuhusu uvumi wa kuwaniwa na Manchester United. ***(Standard)***

### ANCELOTTI KUJIFUNGA MADIRD

CARLO Ancelotti anaweza kusaini mkataba mpya na Real Madrid, huku klabu hiyo ikionyesha kuridhishwa na mwenendo wa raia huyo wa Italia hapo Bernabeu. ***(Marca)***

### EGAN ATAJWA WEST HAM

KLABU ya West Ham inataka kumsajili mlinzi wa Sheffield United na Ireland, John Egan mwenye umri wa miaka 29, kwa pauni milioni 12 Januari. ***(Sun on Sunday)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# MARTIAL AWASHUTUMU MOURINHO, SOLSKJAER

**MANCHESTER,** England

ANTHONY Martial amewashutumu makocha wa zamani wa Manchester United, Jose Mourinho na Ole Gunnar Solskjaer, kwa kumtendea vibaya wakati wa utawala wao pale Old Trafford.

**Fowadi huyo Mfaransa alikua chipukizi ghali zaidi katika historia wakati alipokamilisha uhamisho wake Septemba 2015 wenye thamani ya pauni milioni 58 kutoka Monaco.**

Alisajiliwa na Louis van Gaal, alitumia chini ya mwaka mmoja kucheza chini ya Mholanzi huyo, ambaye alisema alikuwa na "uhusiano naye mzuri".

Mourinho alikuwa mrithi wa Van Gaal, aliyeteuliwa Mei 2016, na Zlatan Ibrahimovic alikuwa miongoni mwa wachezaji wa kwanza kusajiliwa na bosi huyo mpya. Kwa mujibu wa Martial, matatizo yake na Mourinho "yalianza na namba ya jezi", akisema bila kupenda aliitoa namba tisa kwa nyota wa Sweden, Ibrahimovic.

"Wakati wa likizo, (Mourinho) ananitumia ujumbe kuniuliza kama ninataka kubadilisha namba tisa na nivae namba 11, akinieleza kuwa ni nzuri kwa sababu ni ya gwiji Ryan Giggs," alisema Martial akiliambia jarida la France Football.

"Nikamwambia kwamba ninamheshimu sana Giggs, lakini napenda kubaki na namba tisa. Na niliporudi kwenye klabu, jezi yangu ilibadilishwa na kupewa namba 11. Hakuwa na heshima ya moja kwa moja kwangu."

**●●● Alininyang'anya jezi na kumpa Ibrahimovic, hakuwa na heshima ya moja kwa moja kwangu...**

Martial alisema Mourinho, ambaye sasa ni bosi wa AS Roma, alianza kutumia "maneno madogo, kama vile alivyokuwa akifanya kwa Karim Benzema kule Real (Madrid)".

"Alijua kwamba nilikuwa na umri wa miaka 20 wakati huo, na ningesema kitu ningeonekana mimi ni kijana nisiye na heshima, kwa hiyo sikusema chochote."

Martial akajikuta akipoteza nafasi yake kwa mchezaji mwingine mpya, Alexis Sanchez, ambaye alijiunga na United akitokea Arsenal katikati ya msimu wa 2017-18.

"Ulikuwa msimu wa kuelekea Kombe la Dunia, na ilinigharimu sana mwishoni maana sikupata nafasi kwa timu ya Ufaransa," alisema Martial.

Mourinho alitimuliwa na United Desemba 2018, huku Solskjaer akiingia kama mrithi wake.

Martial alimaliza msimu wa 2019-20 kama mfungaji bora wa United akiwa na mabao 23, lakini amedai baadaye Solskjaer alimsimamia vibaya baada ya msimu huo.

Mara tu baada ya kutimuliwa kwa Solskjaer Novemba 2021, Martial alitolewa kwa mkopo kwenda Sevilla, ambapo alifunga mara moja katika mechi 12. Martial alisema alikuwa na majeraha ya mara kwa mara wakati wa utawala wa Solskjaer, akidai kocha huyo alishindwa kuweka wazi hilo.

"Kocha hakuwahi kujisumbua kuviambia vyombo vya habari," alisema Martial, ambaye bado ni mchezaji wa United. "Ni wazi, niliishia kuumia kabisa na niliporudi sikucheza tena."

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
EMPOLI
VERSUS
ROMA
1 | 4.41
X | 3.76
2 | 1.70

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BENZEMA KUREJEA DHIDI YA ATLETICO




**MADRID,** Hispania

KARIM Benzema atakosa mechi mbili zijazo za Real Madrid, lakini anaweza kurejea kwenye mchezo wa dabi na Atletico Madrid, kwa mujibu wa Carlo Ancelotti.

Benzema alitolewa nje akiwa na jeraha la goti wakati Madrid ikishinda mabao 3-0 dhidi ya Celtic katika mchezo wa ufunguzi wa makundi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumanne, na ilihofiwa kwamba angekaa nje ya dimba kwa muda mrefu.

Hata hivyo, Ancelotti ameonekana kuondoa hofu hiyo katika mkutano na waandishi wa habari akisema mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa anaweza kurejea baada ya wiki moja tu.

Baada ya Mallorca, Madrid wanaikaribisha RB Leipzig kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kabla ya kuivaa Atletico Jumapili ijayo.

"Hatutamlazimisha Benzema," alisema kocha Ancelotti. "Hakika hatacheza dhidi ya Leipzig, lakini basi tutaona kwenye dabi.

"Ikiwa hawezi kucheza (dhidi ya Atletico), hatakwenda Ufaransa (kwa mapumziko ya kimataifa)."

Benzema alibadilishwa baada ya dakika 30 pale Parkhead na Eden Hazard, ambaye alifunga bao la tatu katika ushindi huo.




## 'Neymar kanipeleka Barca'

**BARCELONA,** Hispania

RAPHINHA aliambiwa na fowadi wa zamani wa Barcelona, Neymar, kwamba hatajutia kuhamia Camp Nou, na winga huyo wa zamani wa Leeds United, akaridhika na uamuzi wake wa kuikataa Chelsea.

Mchezaji huyo mpya wa 'Blaugrana' ana bao moja na asisti moja katika mechi zake nne za kwanza kwa wababe hao wa Katalunya.

Raphinha alikuwa akihusishwa na Chelsea, lakini alitafuta ushauri kutoka kwa mchezaji mwenzake wa Brazil, Neymar ambaye alishinda mataji mawili ya LaLiga, matatu ya Copa del Rey na Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kipindi cha miaka minne akiwa na Barca kati ya mwaka 2013 na 2017.

"Nilizungumza mengi na Neymar. Aliniambia kwamba ikiwa ningekuja Barcelona basi sitajuta," alisema Raphinha akiliambia La Vanguardia. "Na alikuwa sahihi."

Akielezea kwa nini aliidharau Chelsea, Mbrazil huyo aliongeza: "Ndoto yangu ilikuwa kuvaa jezi ya Barcelona. Hii ni klabu ambayo nimekuwa naipenda tangu nikiwa mdogo sana.

HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# SBL YAAHIDI KUENDELEA KUSAIDIA MAENDELEO YA MCHEZO WA SOKA

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU chache tangu kumalizika kwa Mkutano Mkuu wa 44 wa Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), uliofanyika jijini Arusha, Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), imesema itaendelea kuunga mkono jitihada za kuendeleza mchezo huo wenye wapenzi wengi zaidi duniani.

**Ikiwa ni mara ya kwanza kufanyikia Tanzania, mkutano huo mkubwa ulizileta pamoja nchi 52 wanachama wa CAF huku ukihudhuriwa na viongozi wenye dhamana kubwa ya soka duniani ikiwa ni pamoja na Rais wa Shirikisho la Soka Duniani (FIFA), Gianni Infantino na Rais wa CAF, Patrice Motsepe.**

SBL inaunga mkono kauli aliyotoa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kwenye hotuba yake wakati akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan kwenye ufunguzi wa mkutano huo ambapo alisema serikali inafanya jitihada kubwa kuwekeza na kujenga mazingira mazuri kwa ajili ya ukuaji wa mchezo wa soka.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Mahusiano kwa Umma wa SBL, John Wanyancha, Serengeti imekuwa ni mdau mkubwa wa maendeleo ya michezo na imekuwa ikifadhili michezo mbalimbali ikiwamo soka.

Wanyancha amesema, kupitia udhamini wa Bia ya Serengeti Lager, Timu ya Taifa 'Taifa Stars' iliweza kufuzu mashindano makubwa kabisa barani Afrika ya Mataifa ya Afrika (AFCON), yaliyofanyika nchini Misri mwaka 2019 na kwamba ilifuzu ikiwa ni miaka 39 tangu ifuzu kwa mara ya mwisho.

Kabla ya kufuzu mashindano hayo makubwa barani Afrika, SBL kupitia kinywaji chake cha Serengeti Lager ilisaini mkataba wa miaka mitatu na TFF ambapo ilitoa kiasi cha Sh. bilioni 2.1 kuidhamini Taifa Stars katika kipindi cha miaka mitatu, udhamini ambao ulikuwa na mafanikio makubwa kwa timu hiyo.

Oktoba mwaka 2020, Bia ya Serengeti Premium Lager (SPL), iliingia makubaliano na kusaini mkataba na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa ajili ya kuidhamini Taifa Stars kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.

Wakati wa kutiliana saini mkataba huo, rais wa TFF, Wallace Karia alinukuliwa akisema SBL kupitia chapa ya Serengeti imekuwa ni mfano wa kuigwa katika kuchangia maendeleo ya michezo na kuyataka makampuni mengine kuiga mfano.

Mkataba huo unaogharibu shilingi bilioni tatu, umesainiwa baada ya ule wa awali uliosainiwa mwaka 2017, kufikia ukomo katikati ya mwaka 2020 huku timu ikijivunia mafanikio mengi katika kipindi cha udhamini.

SBL kupitia Bia ya Serengeti Lite pia imekuwa mdau mkubwa wa soka la wanawake. Serengeti Lite ndiyo mdhamini wa kwanza na wa pekee kwa ligi ya wanawake tangu ianzishwe hapa nchini. SBL pia imekuwa ikisaidia michezo mingine ikiwamo gofu na riadha.

**TUNAJALI...**




Meneja Masoko wa GSM Tanzania, Rukia Yazid (kulia), akimkabidhi Mkuu wa Kituo cha Goodwill and Humanity Foundation, Muhdhari Idarusi, nazi, sukari pamoja na bidhaa zingine ikiwa ni baadhi ya mahitaji ya vyakula yaliyotolewa mwishoni mwa wiki kama msaada. GSM Tanzania na wachezaji wa Coastal Union nyuma waliovaa jezi nyekundu, walitembelea kituo hicho kilichoko jijini Tanga kutoa misaada. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Coastal, Polisi zaweka rekodi Ligi Kuu*

**Na Adam Fungamwango**

MECHI kati ya Coastal Union na Polisi Tanzania iliyochezwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha juzi, imeweka rekodi ya kuwa mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu kwa timu kutoka bila kufungana.

Coastal ambayo ilianza maisha mapya bila kocha wao, Juma Mgunda, aliyetimkia Simba, ilicheza kwenye uwanja huo ikihesabika kikanuni kuwa wa nyumbani dhidi ya Polisi Tanzania ambayo nayo inautumia kama uwanja wake wa nyumbani.

Inakuwa ni suluhu ya kwanza kwenye Ligi Kuu ambayo imepatikana raundi ya tatu, kwani mechi zote zilizochezwa tangu kuanza kwake, imeshuhudiwa timu zikishinda au sare ya mabao na hakukuwa na suluhu yoyote.

Kabla ya mechi za jana kati ya Singida Big Stars dhidi ya Dodoma Jiji na Namungo dhidi ya Ruvu Shooting, ni Mtibwa Sugar tu iliyopata ushindi kwenye mechi za raundi ya tatu ya Ligi Kuu.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATATU - 12/09/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 5599 | Vorskla Poltava vs Oleksandria | 2.09 | 3.48 | 2.99 |
| 15:00 | 3145 | FC Ingulets vs FC Minaj | 2.45 | 3.04 | 2.75 |
| 16:00 | 3141 | Pyunik Yerevan vs Bkma Yerevan | 1.34 | 4.52 | 7.66 |
| 17:00 | 4406 | Javor Ivanjica vs Radnik Surduluca | 1.76 | 3.54 | 4.03 |
| 17:30 | 2341 | Indjija vs FK Zeleznicar Pancevo | 2.18 | 3.00 | 3.45 |
| 17:30 | 5768 | Ida-Virumaa FC Alliance vs FC Elva | 8.07 | 5.65 | 1.30 |
| 18:00 | 5791 | CS Mioveni vs Universitatea Cluj | 2.94 | 2.89 | 2.54 |
| 19:00 | 1668 | Olympiakos Nicosia vs AEL Limassol | 3.03 | 3.23 | 2.32 |
| 19:00 | 2139 | Chrobry Glogow vs Resovia Rzeszow | 2.21 | 3.24 | 2.95 |
| 19:00 | 2732 | Stabaek vs Raufoss | 1.42 | 4.53 | 5.72 |
| 19:00 | 2848 | FK Vozdovac vs Radnicki Nis | 2.21 | 3.19 | 2.99 |
| 19:00 | 3158 | Mjondalen vs Skeid Fotball | 1.87 | 3.58 | 3.48 |
| 19:00 | 3290 | Kongsvinger IL vs Kfum Oslo | 2.70 | 3.34 | 2.33 |
| 19:00 | 3340 | Bnei Yehuda vs Hapoel Petah Tikva | 2.67 | 2.87 | 2.87 |
| 19:00 | 3732 | Besiktas vs Basaksehir | 1.87 | 3.46 | 3.96 |
| 19:00 | 4032 | Rail Club de Kadiogo vs Asante Kotoko | 2.31 | 2.90 | 3.10 |
| 19:00 | 4342 | PAOK vs Lamia | 1.26 | 5.45 | 10.09 |
| 19:00 | 4613 | Brann vs Grorud IL | 1.01 | 12.73 | 48.97 |
| 19:00 | 5379 | FK Panevezys B vs FK Banga B | 1.58 | 4.03 | 4.53 |
| 20:00 | 1453 | Verl vs Meppen | 2.32 | 3.29 | 2.89 |
| 20:00 | 1684 | Viborg FF vs Horsens | 1.77 | 3.60 | 4.30 |
| 20:00 | 1827 | Trelleborgs FF vs Orgryte IS | 1.93 | 3.61 | 3.76 |
| 20:00 | 1906 | Jagiellonia vs Stal Mielec | 1.74 | 3.62 | 4.01 |
| 20:00 | 2720 | Altinordu vs Pendikspor | 2.50 | 3.24 | 2.55 |
| 20:00 | 3314 | Kalmar vs BK Hacken | 2.90 | 3.34 | 2.20 |
| 20:00 | 4658 | CF Estrela vs Viseu | 2.22 | 3.23 | 3.08 |
| 20:10 | 4104 | IFK Goteborg vs Helsingborg | 1.61 | 3.74 | 4.72 |
| 20:30 | 5247 | Beitar Jerusalem vs Hapoel Katamon | 2.23 | 3.09 | 3.05 |
| 21:00 | 1666 | Jong AZ Alkmaar vs PEC Zwolle | 4.87 | 4.18 | 1.56 |
| 21:00 | 2370 | Diosgyori Vtk vs MTK Budapest | 3.19 | 3.87 | 1.89 |
| 21:00 | 3116 | Almere City vs FC Eindhoven | 2.31 | 3.34 | 2.84 |
| 21:00 | 3149 | Baltika Kaliningrad vs FC Dynamo-Makhachkala | 1.62 | 3.47 | 5.09 |
| 21:00 | 3246 | Roda Kerkrade vs De Graafschap | 2.08 | 3.57 | 3.08 |
| 21:00 | 4372 | Steaua Bucuresti vs Voluntari | 1.58 | 3.74 | 5.59 |
| 21:00 | 5127 | Jong Utrecht vs ADO Den Haag | 2.94 | 3.49 | 2.18 |
| 21:00 | 5547 | Jong Ajax vs NAC Breda | 1.95 | 3.74 | 3.29 |
| 21:00 | 5577 | Sacachispas FC vs Flandria | 2.75 | 2.90 | 2.55 |
| 21:00 | 5640 | Jong PSV vs Den Bosch | 1.81 | 3.84 | 3.69 |
| 21:30 | 1557 | Adana Demirspor vs Trabzonspor | 2.25 | 3.47 | 2.92 |
| 21:30 | 2097 | AZ Picerno vs Foggia | 2.88 | 3.13 | 2.48 |
| 21:45 | 3306 | Empoli vs Roma | 4.41 | 3.76 | 1.70 |
| 21:45 | 5848 | Metz vs Guingamp | 2.13 | 3.20 | 3.35 |
| 22:00 | 1152 | Red Star vs Paris 13 Atletico | 1.68 | 3.48 | 4.96 |
| 22:00 | 2699 | Eibar vs Granada | 2.34 | 3.04 | 3.09 |
| 22:00 | 3573 | Guabira Montero vs Clube Desportivo Aurora | 1.61 | 3.63 | 4.91 |
| 22:00 | 5209 | Almeria vs Osasuna | 2.66 | 3.07 | 2.71 |
| 22:15 | 4711 | FC Vizela vs GD Estoril | 2.23 | 3.17 | 3.22 |
| 23:00 | 3805 | Sarmiento Junin vs Independiente | 2.80 | 2.90 | 2.51 |
| 23:00 | 5492 | Tigres FC (COL) vs Orsomarso | 1.69 | 3.34 | 4.78 |
| 23:30 | 1544 | Sport Huancayo vs Univ San Martin | 1.20 | 5.93 | 9.88 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumatatu Septemba 12, 2022

Nipashe



Martial awashutumu Mourinho, Solskjaer UKURASA 21

LA KIDEONI...



Mshambuliaji wa Simba, Moses Phiri, 'akibinjuka' kuifungia timu yake bao la kwanza wakati ikishinda 2-0 dhidi ya Nyasa Big Bullets kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Bingu wa Mutharika nchini Malawi juzi. **PICHA: SIMBA**

## Nabi alia na nafasi Yanga

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema ana kazi kubwa ya kuimarisha safu yake ya ushambuliaji hasa katika michezo ya kimataifa katika hatua zinazofuata za michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, CAF.

Kauli hiyo aliitoa juzi, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam baada ya kupata ushindi wa mnono wa mabao 4-0 dhidi ya Zalan FC katika mchezo wa awali wa michuano hiyo huku kipindi cha kwanza wakishindwa kuzitumia nafasi nyingi walizotengeneza.

Yanga inatarajia kucheza mchezo wa marudiano dhidi ya Zalan FC Jumamosi wiki hii na mshindi wa jumla atatinga raundi ya kwanza kukutana na ama St. George ya Ethiopia au Al Hilal ya Sudan.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema mechi haikuwa rahisi kipindi cha kwanza kwa sababu walicheza na timu hawaifahamu ubora na madhaifu yao, hivyo kupata wakati mgumu wa kufumania nyavu dakika 45 za kwanza.

"Ambundo (Dickson), alicheza vizuri na kukosa nafasi ya wazi pia alikosa kujiamini na tuliona madhaifu yao, hivyo tukamtoa na nafasi yake kuchukuliwa na Nkane (Denis) ambaye tulimpa jukumu la kupeleka mashambulizi ya pembeni, kutafuta matokeo," alisema.

# PHIRI AAHIDI 'MAUAJI', MGUNDA AFUNGUKA

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

## ●●● Watamba cheche kuwaka zaidi kwa Mpaka CAF, Barbara na Tshabalala wasema...

KAIMU Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, ameonyesha kufurahia ushindi wa mabao 2-0 kwenye mechi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Nyasa Big Bullets ya Malawi, timu yake ikiwa ugenini baada ya kueleza kuwa kazi haijaisha, huku Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Barbara Gonzalez akiwasifu makocha wazawa kwa kuiongoza vema timu hiyo.

**Mbali na hayo, straika Moses Phiri aliyefunga bao la kwanza kwenye mechi hiyo, aliwasifu wanachama na mashabiki wa Simba kwa kusafiri kwa umbali mrefu kuwapa sapoti, akiahidi hatowaangusha kwenye mechi ya marudiano.**

Wote hao walizungumza juzi baada ya Simba kumaliza dakika 90 kwenye Uwanja wa Bingu Mutharika kwa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya wenyeji hao, yakiwekwa wavuni na Phiri, pamoja na nahodha wa kikosi hicho, John Bocco.

"Nina furaha kwa sababu nimeshinda ugenini, lakini mechi haijaisha mpaka iishe kule nyumbani, tumeyaona makosa ya wachezaji, tunakwenda kuyarekebisha ili tushinde. Kwenye mechi chochote kinaweza kutokea, iwe nyumbani au ugenini, siwezi kuidharau Nyasa Big Bullets. Muhimu kwa sasa ni kwamba tunaongoza, lakini tuna mechi nyingine nyumbani na tuna mtaji wa mabao 2-0," alisema Mgunda ambaye ilikuwa ni mechi yake ya kwanza kuiongoza Simba kwenye maisha yake ya soka.

Alimsifu kocha aliyemkuta Selemani Matola, akidai kuwa amempa mwanga wa kuwafahamu wachezaji na kuwatumia.

"Nimeipokea timu muda mfupi sana kabla ya mechi, lakini mwalimu niliyemkuta nimeshawahi kufanya naye kazi timu ya Taifa, Taifa Stars miaka miwili au mitatu, najua uwezo wake, nilianzia pale aliponiambia timu ikoje. Amenisaidia kunipa mwanga kuhakikisha timu inafanya vizuri," alisema kocha huyo wa zamani ni mchezaji wa Coastal Union.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Barbara aliwasifu wachezaji na benchi lote la ufundi kwa kuiheshimisha Simba na nchi kwa ujumla.

"Tunashukuru walimu na wachezaji kuiheshimisha klabu kupambana, kucheza kwa nembo ya Simba na Tanzania, bado tuna safari ndefu kuna dakika 90 za nyumbani na tunategemea kuona ushindi zaidi ili twende kwenye raundi nyingine, nimefurahi kuona makocha Watanzania wameleta ushindi kwenye mechi ya ugenini.

"Pia nitoe pongezi kwa wanachama na mashabiki na kuwashukuru pia kwani wamesafiri saa 40, na zaidi ya watu 150 kutoka Tanzania wamekuja hapa kuipa sapoti timu, wameonyesha mapenzi ya dhati na imetusaidia, ndiyo maana unaona hata wachezaji wetu wamepambana sana kwa sababu walikuwa wanasikia makelele na ngoma za nyumbani kutoka kwa mashabiki tokea hotelini hadi uwanjani," alisema.

Phiri, mfungaji wa bao la kwanza alisema huo ni mwanzo tu, huku akikiri kuwa mashabiki wengi waliojitokea kuwashangilia walikuwa chachu ya ushindi huo.

"Nafikiri huu ni mwanzo mzuri kwetu hasa kushinda mechi ya ugenini, tumekuja kushinda na lengo letu limetimia.

"Nashukuru kwa kufunga na kwa hii imekuja kwa ushirikiano wa wachezaji wenzangu, najua kuna mashabiki wengi walikuja kutoka Tanzania kutupa sapoti, hiyo ilikuwa sababu ya kutusukuma na kujituma zaidi kwenye mechi hii na zingine zitakazokuja, nao wanatakiwa kuendelea kuja kutushangilia, hatutowaangusha," alisema Mzambia huyo.

Kwa upande wa nahodha Msaidizi wa Simba, Mohammed Hussein 'Tshabalala', alisema hawajamaliza kazi, wanarudi imara kwa ajili ya kutafuta matokeo chanya katika michezo iliyopo mbele yao ukiwamo huo wa marudiano.

Alisema baada ya kumalizana na Big Bullets sasa akili na nguvu zao wanaziielekeza kwenda kutafuta pointi tatu katika mchezo ujao dhidi ya Tanzania Prisons ili kuendelea kubaki kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu.

"Ushindi muhimu ugenini tumejiandaa vema kwa mechi zetu zijazo ili kufikia malengo, asanteni mashabiki wetu kwa dua zenu na wale mliotoka Tanzania hadi Malawi sapoti yenu ilikuwa kubwa sana".

Kikosi cha Simba baada ya kurejea kitashuka Uwanja wa Sokoine Jumatano kuvaana na Mbeya City kabla ya kurejea Dar es Salaam kuisubiri Nyasa Big Bullets katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >